

# MWONGOZO WA HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

Cultural Survival | First Peoples Worldwide, University of Colorado Boulder | SIRGE Coalition, Securing Indigenous Peoples' Rights in the Green Economy | BATANI | EARTHWORKS | Gesellschaft für bedrohte Völker




# MWONGOZO WA HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

Imeandikwa na Uhai wa Kitamaduni na Watu wa Kwanza Ulimwenguni Pote, kwa msaada kutoka kwa Kulinda Haki za Watu wa Asili katika Uchumi wa Kijani.(SIRGE) Muungano. Kwa shukrani kwa wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Muungano wa SIRGE na viongozi wengine wa asili kutoka kote ulimwenguni ambao ilichukua muda kukagua mwongozo huu na kuwapa vipawa mitazamo na utaalamu wao. Wachangiaji: Rachael Knight, Galina Angarova, Kate R. Finn, Edson Krenak, David Gordon. Vielelezo: Özgür Uğuz, ozguruguz@gmail.com. Mpangilio: Tania Dunster / Onehemisphere, contact@onehemisphere.se. Picha: Shutterstock. Mhariri: Jenn Goodman. Kurasa: 56. Eneo la Kijiografia: Ulimwenguni. Tarehe ya Kuchapishwa: Septemba 2023. Imechapishwa na Cultural Survival www.culturalsurvival.org, 2067 Massachusetts Avenue Cambridge, MA 02140, Marekani.

Cultural Survival

First Peoples Worldwide
UNIVERSITY OF COLORADO BOULDER

SIRGE COALITION
SECURING INDIGENOUS PEOPLES' RIGHTS IN THE GREEN ECONOMY

# Yaliyomo


Barua kutoka kwa Wakurugenzi 4
Muhtasari wa rejea kwa ufupi 6
Utangulizi 8

01 **HAKI YA WATU WA ASILI KUJULISHWA,KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABAL YA KUFANYA MAAMUZI**
(Kwa Kiigereza ni FPIC) 10
Nini maana ya FPIC 11
Watu wa Asili na taratibu zao za Kimila/Miiko 12

02 **MAADADALIZI YA AWALI: KABLA YA KUSHIRIKI ANZA YAFUATAYO** 18
Fanya maandalazi ya ndani 20
Elezea taratibu zenu za Kimila 23
Tafuta ushauri wa kisheria na wakitaalam Jifunze kuhusu 26
uwekezaji wa mradi na vyanzo vyake vya mapato 27

03 **TARATIBU ZA MAJADILIANO** 28
Mchague mwakilishi wa Jamii kwenye mazungumzo na majadiliano yote na kuwaanda kwa jukumu hilo 30
Mkubaliano namza zoezi itakavyoendeshwa 31
Hifadhi kumbukumbu ya zoezi kwa muda halisi 32
Hakikisha una uelewa wa kutosha 33
Jadiliana mabadiliko ya mradi husika kuepusha athari na hatari zake 35
Mjadiliane ni faida zipi mtapata kwa serikali au mwekezaji ikiwa mtakubaliana na mradi 36
Fanyeni maamuzi 37

04 **BAADA YA MAAMUZI: HATUA ZINAZOFUATA** 40
Ikiwa mmekataa: Hakikisha kukataa kwenu kumekubaliwa 41
Ikiwa mmekubali: Chukueni hatua makhususi kulinda haki zenu 42

---

**VIAMBATANISHO** 49
**Kiambatanisho A:** Tafsiri/maneno muhimu 49
**Kiambatanisho B:** Msimamo wa kisheria kwa ( FPIC) 50
**Kiambatanisho C:** Kuthaminisha thamani ya rasilimali ya jamii uliopo katika ardhi na uoto wa asili 52
**Kiambatanisho D:** Kuwa na mtazamo wa mbali wa jamii yako katika siku zijazo 54
**Kiabatanisho E:** Idadi ya Mashirika na vyombo vya kimataifa kwaajili ya Watu wa Asili Watu wa Asili kuwasiliana nao kwa msaada zaidi 55
**Kiambatanisho F:** Idadi ya Mapendekezo muhimu 56



Uzalishaji na usambazaji wa taarifa zilizomo katika Mwongozo huu wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiari kabla ya Kufanya Maamuzi unaruhusiwa ikiwa chanzo kitatambuliwa na kutajwa wazi. Hata hivyo, tafsiri ya mwongozo huu kwenda lugha zingine Pamoja na unakili wake hautoruhusiwa bila kwanza kibali kutoka kwa Cultural Survival.

# BARUA KUTOKA KWA WAKURUGENZI

**Upatikanaji wa Haki ya Kujitawala ya Watu wa Kiasili: Mwongozo kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi** umeandikwa kwa ajili ya viongozi wa Jamii za asili. Tumekusikia: hakuna kitu muhimu zaidi kuliko kupata haki za kibinafsi na za jamii yenu yote kwa mustakabali bora unaohakikisha ustawi wa kitamaduni, kiroho, kimazingira na kiuchumi. Tumewasikia pia kwamba utekelezaji wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kama ilivyofafanuliwa na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu wa Asili ni mgumu na wakati kwa njia ya kutia hofu.

Tunataka kueleza bayana kwamba Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi inakusudiwa kulinda kwa ukamilifu haki za Watu wa Asili mbali ya ardhi na maliasili. Tunalenga kulinda pia haki za lugha, elimu, Maarifa ya Jadi, na mali za kitamaduni na ubunifu wa kiakili. Vipaumbele vyenu mlivyojiamulia lazima viwe msingi wa majadiliano na taasisi za nje. Tumeandaa mwongozo huu kwa ajili ya kuwasaidia katika kusimamia haki na vipaumbele vyenu na kuwasaidia kutekeleza vyema Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kwa kuongozwa na mifumo, tunu, mila na maono yenu kwa vizazi vijavyo.

Kwa zaidi ya miaka 75 ya uzoefu wa pamoja kati ya mashirika yetu, tumefanya kazi pamoja na kuwaunga mkono viongozi wa Jamii za asili katika kupigania utu na kudumisha haki za Watu wa Asili na kujiamulia kuhusu mustakabali wao. Tangu Azimio lilipopitishwa mwaka 2007, tumejifunza mengi kutokana na uzoefu. Mara nyingi tunazungumza na Watu wa Asili duniani kote kuhusu utekelezaji wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi katika mazingira tofauti wakikabiliana na mifumo tofauti ya kisheria na kisiasa, hali tofauti za utambuzi rasmi na usio rasmi wa kisheria, kanuni mbalimbali zinazohusu umiliki wa ardhi na uziduaji wa rasilimali, na tofauti za muktadha wa kijamii na kitamaduni.

Tunatambua ugumu wa utekelezaji wa Haki ya Kujulishwa, Mwongozo huu umeandikwa ili kuonyesha uzoefu wa Watu wa Asili kutokana na mazingira tofauti ya kisheria, kisiasa, na kijamii na kitamaduni kote ulimwenguni. Mwongozo huu unaonesha mbinu bora za Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi katika muktadha wa miradi ya uwekezaji, hasa ile inayoathiri ardhi, maeneo na rasilimali za Watu wa Asili. Pia unaonesha mikakati ambayo Watu wa Asili wanaweza kutumia katika Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi katika jamii na washirika wa kutoka nje na hitaji la dharura la kutafuta suluhisho na vipaumbele vya Watu wa Asili. Tafsiri ya utajiri wa watu wa asili huenda mbali zaidi ya fursa za kiuchumi na mafanikio ya kifedha. Tafsiri ya watu wa asili kuhusu utajiri ni pana zaidi na inajumuisha kuwa na watu wenye afya njema, jamii dhabiti, na mifumo himilifu ya kiikolojia. Tunajua vipaumbele vya viongozi wa jamii za asili ni kupigania ustawisha wa jamii zao. Pia tunajua kuna tafsiri nyingi za Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kama ambavyo kuna makundi tofauti ya jamii za asili.

Muhimu zaidi, mwongozo huu unapendekeza kwamba Watu wa Asili mtengeneze kwa umakini itifaki zenu zinazohusu HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI, mkionesha vipaumbele mahususi vinavyoakisi mifumo yenu ya utawala na maamuzi shirikishi. Ni vema Itifaki hizi ziandikwe mapema kabla ya kupokelewa kwa maombi ya mwekezaji ili itifaki zenu zitumike kuongoza majadiliano, kuliko kufuata taratibu zilizowekwa na serikali au mwekezaji.

Hizi ni zama muhimu kwa Watu wa Asili kujitawala. Muongo huu ujao lazima utambulike kwa kuonesha heshima kwa viongozi wa WWatu wa Asili, kwa kupitia ujumuishaji wa itifaki za HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI za Watu wa Asili katika sekta binafsi na za umma kote ulimwenguni. Tunatumaini kuwa mwongozo huu utakuwa mwanzo wa majadiliano kuhusu namna ya kusimamia vipaumbele vyenu kuhusiana na HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI ndani na nje ya jumuiya zenu.

Kwa mshikamano,



**Galina Angarova** (Buryat)
Mkurugenzi Mtendaji, Uhai wa Utamaduni Mwenyekiti mwenza wa Kamati ya Utendaji, Kupata Haki za Watu wa Asili katika Muungano wa Uchumi wa Kijani.



**Kate R. Finn** (Osage)
Mkurugenzi Mtendaji, First Peoples Worldwide Mwenyekiti mwenza wa Kamati ya Utendaji, Kupata Haki za Watu wa Asili katika Muungano wa Uchumi wa Kijani.



Kiongozi wa Jamii ya Asili akiwasilisha mada kuhusu maazimio ya kisera juu ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kwa niaba ya wadau kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Benki.

# MUHTASARI MFUPI WA MAREJEO

Watu wa Asili wanayo haki ya kuamua kinachoendelea katika ardhi yao. Mchakato wa majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi unatakiwa kufanyika kabla ya kuanza mradi wowote ule ambao unaweza kuathiri ardhi, himaya, na rasilimali ambazo Watu wa Asili wanamiliki kimila, wanashikilia, au kuzitumia. Haki ya Kujulishwa, Kuelewa Na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi inajumuisha: 1) Mchakato wa majadiliano na maelewano (kuombwa ushauri, kuuliza maswali, kupatana, kutenga muda wa kutosha kuuelewa mradi vizuri); na 2) haki ya kuridhia au kutoridhia wakati wa majadiliano au baada ya majadiliano. Haki ya Kujulishwa, Kuelewa Na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi inatokana na haki ya Watu wa Asili ya kujiamulia mambo yao wenyewe. Sehemu ifuatayo inatoa muhtasari wa namna jamii yenu inaweza kujiandaa, kujadiliana, na kukamilisha mchakato wa

kusimamia Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Mwongozo kamili unaeleza kwa kina kila hatua.

## MAJADILIANO HUANZA KABLA YA HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

Wakati jumuiya yenu inatembelewa na wawekezaji na/au maofisa wa serikali wanaotafuta ardhi na rasilimali, ni vyema kuchukua hatua mbalimbali, zikiwemo:

1. **Fanya jitihada za kuhakikisha kuna mshikamano kwenye jamii** kwa kufafanua na kukubaliana juu ya vipaumbele vya jamii yenu; kuimarisha umoja wa jamii; kutoa nafasi kwa maoni tofauti; na kuhakikisha kuwa kunakuwepo na mifumo mizuri ya kutatua migogoro.
2. **Fanyeni uamuzi wa kuandika itifaki yenu wenyewe za Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi** inyoweka msingi wa namna ambayo majadiliano kuhusu haki hizo yatafanyika kwenye jamii yenu.
3. **Fafanueni mipaka ya ardhi yenu** na weka alama ya maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya kijamii.
4. **Jitahidini kuelewa haki zenu kisheria** kwa mujibu wa sheria za nchi na za kimataifa.
5. **Jifunzeni jinsi wawekezaji na maofisa wa serikali wanavyothaminisha ardhi na rasilimali zenu, na kuelewa pia thamani ya ardhi na rasilimali zenu wenyewe, ili muweze kuwasilisha hili kwa uwazi kwa wawekezaji na maafisa wa serikali.**
6. **Tafuteni msaada wa kisheria na kitaalamu.**
7. **Jifunzeni kuhusu mnyororo wa uwekezaji wa mradi** ili muwaelewe mnaohusiana nao na namna bora ya kuhakikisha kuwa wahusika hao wanaheshimu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi.

## MCHAKATO WA MAPATANO

**Mara tu baada ya jamii yenu pamoja na wawekezaji na/au maofisa wa serikali kuanza kutafuta ardhi na rasilimali kwa ajili ya mradi uliopangwa wa uwekezaji au miundombinu** anzisheni rasmi mchakato wa majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi, jamii yenu inaweza kuchukua hatua kadhaa, zikiwemo:

1. **Chagueni wawakilishi wa jamii yenu** katika vikao vyote vya majadiliano na maelewano kwa ajili ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi;
2. **Wasilisheni itifaki yenu inayopaswa kwa wawekezaji na maofisa wa serikali mtakaokutana nao** kwa ajili ya kuhakikisha kunakuwepo na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi na **kukubaliana kuhusu namna ya kuendelea na mchakato**;

3. **Wekeni kwenye maandishi masuala ya mchakato** kwa ajili ya kuweka ushahidi ambao mnaweza kuuhitaji baadaye;

4. **Hakikisheni kuwa mnao uelewa wa kutosha** kwa kukusanya nyaraka zote muhimu na kuelewa kuhusu tathmini yoyote ya athari iliyowahi kufanyika.

5. **Jadilianeni kuhusu mabadiliko yanayohitajika kwenye mradi unaopendekezwa** ambayo mnaona ni ya muhimu kwa ajili ya kuepusha hatari na madhara; na

6. **Jadilianeni kuhusu faida na matokeo chanya** ambayo serikali au mwekezaji lazima atoe endapo mtauridhia mradi.

## KUFANYA MAAMUZI

Baada ya jumuiya yenu kupata taarifa zote muhimu na kushiriki kikamilifu katika mchakato wa mashauriano na mapatano na kampuni na/au serikali, mtakuwa tayari kuujadili mradi husika kaika vikao vyenu vya ndani na kuamua kukubalia au kukataa haki yenu yako ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi. **Katika kila kipengele, jumuiya yenu ina haki ya kujiamulia, ikiwa ni pamoja na kuamua namna mtakavyofanya uamuzi**. Mna haki ya kufanya uamuzi kulingana na michakato yenu ya jadi ya kufanya maamuzi. Jumuiya yenu ikishafanya uamuzi, andika jinsi mlivyokubali au uamuzi wenu wa kutoridhia kukiwa na sababu kadhaa, zikiwemo video, picha na karatasi.

## HAKI YA KUFANYA UAMUZI BAADA YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI

### IKIWA MMEKATAA:

**Hakikisheni kuwa uamuzi wenu wa kukataa umekubaliwa.** Ikiwa jamii yenu imeamua kukataa kuridhia, tafuteni mwanasheria wa kusaidia kusimamia haki zenu kwa mujibu wa sheria za nchi husika. Mwanasheria anaweza kuwashauri kuhusu mikakati mbalimbali mnayoweza kuifuata kwa ajili ya kusimamia haki yenu ya kusema hapana.

### IKIWA MMEKUBALI:

1. Itakuwa jambo jema zaidi ikiwa **makubaliano na mapatano yaliyotokana na ridhaa ya jamii yenu yakawekwa katika mkataba wa kimaandishi ambao umeandaliwa na kutiwa saini na wahusika wote.** Tafuta usaidizi na ushauri wa wasaidizi wa kisheria, wanasheria, wataalamu wa kiufundi, na mawakili wengine unapofanya kazi na wawekezaji na/au maafisa wa serikali kuandaa na kukamilisha mkataba rasmi.
2. **Anzisheni mpango wa ufuatiliaji na uzingatiaji wa mkataba** kama sehemu ya makubaliano na mkataba unaohusiana na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi. Na hili linajumuisha vipengele walau vitatu:
   - Mawasiliano ya wazi na majadiliano ya mara kwa mara yenye nia ya kujenga;
   - Haki yenu ya kufuatilia shughuli za mradi katika kipindi chote cha mradi husika;
   - Hatua ambazo mwekezaji na/au serikali itazichukua ikitokea kuna taarifa za uchafuzi wa mazingira, kukiukwa kwa mkataba, na changamoto nyinginezo zinazoweza kuleta madhara kwa jamii yenu.
3. Ikiwa mwekezaji na/au serikali hawatatatua changamoto zilizopo, ukiukaji wa mkataba na/au dhuluma zilizobainishwa, basi jamii yenu ina haki ya kuanzisha utaratibu wa kuwasilisha malalamiko na/au mchakato wa kutatua mizozo. **Hakikisheni kuwa mkataba wenu unajumuisha taratibu za wazi za malalamiko na taratibu za utatuzi wa migogoro.**

# UTANGULIZI

Mwongozo huu umeandikwa ili kusaidia Watu wa Asili wanaotetea ardhi, maeneo na rasilimali zao. Unalenga kutoa mwongozo ulio wa kina kwa viongozi na jamii za watu wa asili kuhusu namna ya kutekeleza Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi. Unajumuisha mapendekezo ya kitaalamu na ya kimkakati kuhusu namna bora ya kuuendana na mifumo ya kimataifa ya mamlaka na fedha ili Watu wa Asili waweze kupata mafanikio wanapokabiliana na mifumo hiyo.

Mwongozo huu umewekwa kwa mpangilio ufuatao:

- **Sehemu ya 1** inafananua maana ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi na kueleza namna watu wa asili wanavyopambana kwa mafanikio kuandika itifaki za haki hizo kwa kutoa mwelekeo wa majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi.
- **Sehemu ya 2** inaeleza hatua za ndani ambazo jamii za asili zinaweza kuchukua kwa ajili ya kujiandaa. Muhimu zaidi ni kuandaa itifaki yenu ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi. Sehemu hii pia inashauri kuhusu kuchukua hatua za kuelewa zaidi kuwahusu wawekezaji/ waandaaji wa mradi kwa ajili ya kujua ni akina nani hasa, na ni nani anayefadhili kazi yao.
- **Sehemu ya 3** inaeleza kile ambacho jamii za asili zinaweza kufanya wakati wa mchakato wa majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi, ikiwa ni pamoja na kupata usaidizi wa kisheria na kitaalamu, kuhakikisha kuwa una taarifa kamili, inayomtaka mwekezaji kupunguza hatari za mradi na kujadiliana faida mtakazopata kutokana na mradi baada ya kuridhia ardhi yenu ichukuliwe.
- **Sehemu ya 4** inaeleza aina mbalimbali za hatua za ufuatiliaji ambazo jamii ya watu wa asili inaweza kuchukua baada ya kukamilika kwa mchakato wa mashauriano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi. Inafafanua kile mnachohitaji kufanya kwa ajili ya kulinda haki zenu ikiwa mliukubali mradi, na kile mnachoweza kufanya ili kutetea uamuzi wenu wa kutoridhia mradi.

Ni matumaini yetu kwamba mtauchukua mwongozo huu na kuutafsiri katika lugha zenu ili jamii zenu ziweze kuusoma na kuutumia kuandaa mijadala na ushirikiano na wawekezaji na serikali kuhusiana na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi. Kwa ajili ya kupata nakala ya kidijitali ya mwongozo huu ambayo mnaweza kuitumia kwa madhumuni ya kutafsiri tafadhali wasiliana na Cultural Survival kwa **culturalsurvival@cs.org.**



## DOKEZO KUHUSU UCHAGUZI WA MANENO

- Katika mwongozo huu, tunatumia maneno "Jamii ya watu wa Asili" na "jamii" kwa kubadilishana. Mwongozo huu umeandikwa kwa ajili ya kutumika na Watu wa Jamii ya Asili na haukukusudiwa kutumika na jamii zisizo za kiasili. Tunapotumia maneno "Jamii ya watu wa asili" na "jamii," tunamaanisha makundi ya watu ambao wameelezwa na Umoja wa Mataifa kama watu wa asili, yaani: "Wale watu wanaojitambulisha kuwa watu asili, wanaofungamana kwa kiasi kikubwa na maeneo ya watu wa kiasili na maliasili na mwendelezo wa kihistoria kabla ya ukoloni na/au kabla ya walowezi, jamii hizo zina lugha za kipekee, na zimehifadhi asili yao ya kijamii, kitamaduni, kidini, kiuchumi na kisiasa ambazo ni tofauti na za jamii zilizozoeleka ambako wanaishi na kudumisha na kuendeleza kizazi katika mazingira na mifumo ya mababu zao kama watu na jamii iliyo ya kipekee."
    - Tunatambua kwamba ndani ya jamii yoyote ya "Watu wa asili", kunaweza kukawepo vikundi vidogo vidogo vingi. Mwongozo huu haulengi kuangazia utofauti mpana wa jamii za asili. Badala yake, neno "Jamii ya watu wa asili" linakusudiwa kujumuisha mifumo na migawanyiko yote tofauti, inayoingiliana na iliyochangamana ndani ya vikundi.
    - Tunaepuka kutumia maneno 'Watu wa Kiasili' na 'jamii za wenyeji,' kwa sababu jamii z a wenyeji hazina sifa sawa na jamii za asili.
- Katika mwongozo huu, tunatumia neno **"rasilimali"** kumaanisha uwingi wa rasilimali zilizopo ndani ya maeneo ya Watu wa Asili, zinazoonekana na zisizoonekana. Hii ni pamoja na mfumo wa kikolojia wa eneo husika, ukijumuisha mimea, wanyama, madini, maji na udongo. Pia katika kuelezea dhana ya 'rasilimali' tunajumuisha maarifa asilia, ubunifu wa kiakili, na urithi wa kitamaduni.
- Katika mwongozo huu, tunatumia neno **"eneo"** kumaanisha muunganiko na vizazi vya sasa vya Watu wa Asili kwenye eneo la kijiografia, likijumuisha ardhi zote, maji, na mifumo ya kiikolojia iliyomo ndani ya eneo hilo.
- Katika mwongozo huu, tunatumia maneno **"wawekezaji"** na **"wasimamizi wa mradi"** kwa kubadilishana. Kwa maneno haya, tunamaanisha aina tofauti za makampuni, wafanyabiashara, wafadhili wa miradi, na maofisa wa serikali walioko nyuma ya mradi wowote wa miundombinu, uwekezaji, au sera ambayo ina athari yoyote kwa Watu wa Asili.

*Soma Kiambatisho A* kwa maana maelezo zaidi ya maana za maneno.

# HAKI YA WATU WA ASILI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

# 01



Wawakilishi wa Watu wa Asili wakipigania uwepo wa  Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi katika jukwaa la Umoja wa Mataifa.

# Nini maana ya FPIC?

Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi inawahakikishia Watu wa Asili haki ya kuridhia na kutoridhia shughuli zozote zinazoathiri ardhi, rasilimali, na maeneo yao. Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi inatokana na haki ya Watu wa Asili ya kujitambua. Hii inajumuisha na kulinda haki zote za Watu wa Asili, zikiwemo haki za ardhi, haki za kuwa pamoja, haki shirikishi, haki za kitamaduni, haki za kuwa na usalama wa chakula na maji, na nyinginezo nyingi. Kanuni za Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi huunda mfumo mzima wa kufahamisha itifaki, taratibu, sheria na kanuni ambazo Watu wa Asili wanahitaji zitekelezwe na kampuni, serikali, na mataifa mengine huru wakati wa kubuni uwekezaji na uandaaji wa miradi ya miundombinu kwenye ardhi yao.

Mnamo mwaka wa 2007, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha **Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Watu wa Kiasili,** kwa kutambua haki binafsi na za kijamii za watu wa asili ikiwemo Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kama sharti la kuruhusu shughuli yoyote inayoathiri jamii za asili. Kama azimio la Mkutano Mkuu, linabeba makubaliano ya kimataifa juu ya viwango vya chini vinavyohitajika kwa ajili ya kuheshimu haki za Watu wa Asili. **Kila nchi iliyotia saini Azimio hilo inatakiwa kupitisha sheria za kitaifa zinazoipa hadhi ya kisheria.** Azimio linajumuisha vifungu vinavyotambua kuwa ni jukumu la serikali kuwapa watu wa asili ‘Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi katika mazingira yafuatayo:

- Kabla ya watu wa asili kuhamishwa (Kifungu cha 10);
- Kabla ya kutumia mali ya kitamaduni, kiubunifu, kidini na kiroho ya watu wa asili (Kifungu cha 11);
- Kabla ya utekelezaji wa hatua zozote za kisheria au kiutawala zinazoweza kuwaathiri Watu wa asili (Kifungu cha 19);
- Kabla ya kutumia ya ardhi ya Watu wa Asili (Kifungu cha 28);
- Kabla ya kuhifadhi au kutupa taka hatari kwenye ardhi ya Watu wa Asili (Kifungu cha 29); na
- Kabla ya serikali kuidhinisha mradi wowote unaoathiri ardhi, maeneo, na rasilimali za Watu wa Asili, hasa miradi ya kuendeleza, kutumia, kuchimba madini, kusambaza maji, au rasilimali nyingine (Kifungu cha 32).

(***Tazama Kiambatisho B*** kwa ajili ya ufafanuzi wa kina wa sheria na sera za kimataifa, kitaifa, mashirika ya kimataifa, na za tasnia husika zinazoelezea kuhusu Haki ya Watu wa Asili ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi).

Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi inajumuisha:

1. Mchakato wa majadiliano na mazungumzo (kushirikishwa, kuuliza maswali, kuelewana, kutenga muda wa kutosha kuelewa kuhusu mradi unaopendekezwa; na
2. Haki ya kuridhia au kutoridhia wakati au baada ya mchakato wa majadiliano.

**HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI inahitajika kabla ya kupitisha na kuanza kwa mradi** ambayo inaweza kuathiri ardhi, maeneo, na rasilimali zinazomilikiwa, kukaliwa ama kutumika na Watu wa Asili.

Mazungumzo kati ya Watu wa Asili, serikali, na wawekezaji mara nyingi hutokea kukiwa hakuna usawa wa madaraka na kunakuwepo na sera za ukandamizaji. Mchakato wowote unaosimamia haki ya watu wa asili ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi lazima ujumuishe jitihada za makusudi za kusawazisha nguvu za madaraka. Utaratibu huu lazima uruhusu Watu wa Asili kufanya majadiliano huru na ya pamoja na kufikia maamuzi kupitia michakato yao ya kufanya maamuzi. Watu wa asili wana haki ya kufanya maamuzi haya katika mazingira ambayo hayawafanyi wawe waoga, na wapewe muda wa kutosha wa kujadili masuala hayo kwa lugha yao wenyewe na kwa njia inayokubalika kiutamaduni.

**Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi inatokana na haki ya Watu wa Asili ya kujitambua. Hii inajumuisha na kulinda haki zote za Watu wa Asili, zikiwemo haki za ardhi, haki za kuwa pamoja, haki shirikishi, haki za kitamaduni, haki za kuwa na usalama wa chakula na maji, na nyinginezo nyingi.**

**Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi ni mchakato wa kudumu. Kama jamii yenu inauridhia mradi, basi ridha yenu lazima itafutwe kwa kila kipengele au mabadiliko ya kipindi chote cha mradi. Muhimu zaidi ni kuwa hata kama jamii yenu inaridhia, bado mnayo haki ya kuondoa ridhaa yenu wakati wowote.**

Katika sheria za kimataifa, **"Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi"**

inaeleweka kama:

## "UHURU"

"Uhuru" maana yake ni kuridhia kwa hiyari na bila ya shuruti, vitisho, kulaghaiwa, ukatili, au hongo. Ridhaa inayotolewa bila ya vitisho ndiyo pekee inatambulika kama halali. "Uhuru" pia humaanisha:

- Jamii yenu inaweza **kuamua kuhusu mambo ya kuwekwa kwenye mchakato wa kuwa na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi**, ikiwemo idadi ya mikutano, muda na mahali pa mikutano, lugha ya mkutano, na kufanya maamuzi kwa ajili ya kuridhia au kutoridhia, pamoja na kuelewa athari zake kwa jamii yenu na ushiriki huru katika majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi.
- **Wanajamii wote wanashiriki kwa uhuru**.
  Hii ina maana kwamba lazima kuwe na wakati na nafasi kwa wanajamii wote wa asili kuuliza maswali, kueleza upinzani au ukosoaji wao, kusimamia maslahi na mambo wanayopendelea, kutoa mapendekezo, kutoa mrejesho, kueleza jinsi mradi unaopendekezwa utakavyowaathiri, na wazungumze kwa uhuru na bila hofu.
- **Watu wa asili walioathiriwa wana uhuru wa kuanzisha umoja wao,** kuratibu jitihada, kubadilishana taarifa na jamii nyinginezilizoathiriwa, na kutembeleana kwa ajili ya kubadilishana uzoefu kuhusu namna miradi kama hiyo ilivyoathiri jamii nyingine. Mradi unaopendekezwa unaweza kuwa na athari zaidi ya moja kwa jamii za asili. Jamii zote zilizoathiriwa zina haki ya kupigania vipaumbele vyao na kushiriki katika kuratibu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa

## "KABLA YA KUFANYA MAAMUZI"

"Kabla ya kufanya maamuzi" maana yake:

- **Ridhaa yenu lazima ipatikane wakati wa kuandaa mradi, mapema kabisa kabla ya shughuli za mradi kaunza**. Muhimu zaidi, ni kwamba Watu wa Asili walioathiriwa lazima washirikishwe kabla ya serikali kutoa vibali vya "utafiti" na/au leseni ili mkitaka mnaweza kugoma kuridhia shughuli za uchunguzi.
- **Ni lazima mpewe muda wa kutosha wa kukutana na kujadili mradi unaopendekezwa wa uwekezaji au miundombinu kabla ya kufanya uamuzi.** Wawekezaji na maofisa wa serikali lazima waheshimu michakato ya kufanya maamuzi ya jumuiya yenu na kuhakikisha kuwa mnapata muda wa kutosha kwa ajili ya kuelewa kikamilifu taarifa zote muhimu kuhusu mradi uliopendekezwa. Muda unaohitajika utategemea michakato ya kufanya maamuzi ya jumuiya yenu kulingana na desturi zenu.

## "KUFAHAMISHWA"

"Kufahamishwa" ina maana kwamba jamii za asili zina haki ya kufahamishwa kikamilifu kuhusu mradi au uwekezaji uliopangwa. Hii ina maana kwamba serikali na waandaaji wa mradi lazima wawaambie—na wawape nyaraka - kuhusu:

- Aina, ukubwa, madhumuni, na mawanda ya mradi uliopendekezwa, ardhi inayohitajika, maji yanayohitajika, rasilimali zitakazotumika, faida zote zinazotarajiwa kupatikana kwa mwaka, na mipango na maelezo mengine yote.
- Athari na hatari zozote za kiuchumi, kijamii, kitamaduni au kimazingira zinazoweza kujitokeza. Hii inaweza kufanywa kwa njia ya utafiti wa kitaalamu ("tathmini ya athari") wa hatari zote zinazotokana na mradi. Nchi nyingi zina sheria zinazotaka kufanyika kwa tathmini ya athari.
- Mpango wa biashara wa mwekezaji, vibali vyote na leseni zinazotolewa na serikali; orodha ya wafadhili/ wawekezaji wote wa mradi, zikiwemo taarifa za kampuni mama zinazohusiana au kampuni tanzu; na maelezo mengine yote muhimu ambayo mnaweza kuomba.

>> **Taarifa lazima itolewe katika lugha na umbo ambalo jamii yenu inaweza kuelewa kwa urahisi.** Mnayo haki ya kuomba taarifa iwe:

- Katika lugha yenu;
  Inazingatia masuala ya utamaduni;
- Iendane na maeneo yaliyochaguliwa na jamii yenu; na

- Na watu wanaoelewa tamaduni na muktadha wako na wawe wamejiandaa na wenye uwezo wa kujibu kikamilifu maswali yote ambayo jamii yenu itauliza.

>> **Taarifa mnazopewa lazima ziwe sahihi, za uwazi na zinazoeleweka kwa wanajamii wote.** Lazima ziwasilishwe kwa muda wa kutosha ili jamii yenu iweze kuzielewa, kuzichambua na kuzitumia kufanya maamuzi yenu. Uhuru huo lazima uwepo wakati wote wa majadiliano na maelewano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi; endapo kutakuwa na taarifa mpya, au muktadha ukibadilika, jamii yenu ina haki ya kupokea taarifa iliyofanyiwa mabadiliko. **Mnaweza kudai taarifa zote za kiutaalamu zifafanuliwe kwa lugha nyepesi.**

## "RIDHAA"

"Ridhaa" inamaanisha haki ya jamii ya asili kusema kwa uhuru "ndiyo," "hapana," au "ndiyo kwa masharti" kwa mradi au mpango wowote utakaoathiri ardhi, maeneo, rasilimali na maisha yako. Uamuzi wa jamii yenu wa kuridhia au kutoridhia unapaswa kutokana na mchakato wa kujiamulia wenyewe mambo yenu.

>> **Ridhaa siyo suala la mara moja**: Ridhaa inaweza kutolewa au kutotolewa endapo kutakuwa na taarifa mpya au athari mpya zinazojitokeza kadiri mabadiliko yanavyotokea kwenye mradi, na endapo vitendo vya kampuni au serikali vina madhara kwa jamii yenu. Mnaweza pia kudai kuwepo na ridhaa kwa kila hatua ya mradi.

## TOFAUTI KATI YA RIDHAA NA MAJADILIANO

**Majadiliano kuhusu Ridhaa huhusisha mikutano mbalimbali ambayo itaipa jamii yenu taarifa muhimu zitakazowawezesha kupata uelewa wa kutosha juu ya mradi unaopendekezwa na athari zake zinazoweza kujitokeza, ndipo sasa mnafanya uamuzi wa kukubali kwa hiyari au kukataa kuridhia mradi.**

Wakati wa majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi hakikisheni majadiliano hayo yanafanyika ipasavyo, kwa kuwa na "mashauriano" mengi ya kijamii yanayolenga kueleza kwa uwazi kuhusu mradi uliopendekezwa, kutoa nyaraka na taarifa zote za mradi, na kuwapa wanajamii muda na fursa ya kutosha ya kuuliza maswali, kupinga baadhi ya vipengele au mradi wote unaopendekezwa, na/au kujadili masharti yake.

**Jamii yenu lazima itenge muda wa kukutana peke yenu** kupitia nyaraka za mradi, kujadili uwekezaji unaopendekezwa, na kisha kuamua kama mnakubaliana na uwekezaji huo, au mnaukataa, au yafanywe marekebisho fulani katika uwekezaji huo ili muweze kuukubali. Mchakato huo unakamilika mnapowasilisha maamuzi yenu. **Majadiliano yakifanyika vizuri, basi wanajamii wapewe haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi.**



## ITIFAKI ZINAZOHUSU HAKI ZA WATU WA ASLI ZA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

Mwongozo huu wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi umeandaliwa kwa ajii ya kusimamia haki ya Watu wa Asili ya kupigania utambulisho wao**. Jamii ya Asili ina haki ya kuamua kuhusu mchakato wa kupata Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi**, ikiwemo wanavyotaka washirikishwe, namna ya kufanya majadiliano, namna watakavyofanya maamuzi, na kama waamue kuridhia au kutoridhia.

Hata hivyo, imezoeleka kuwa maofisa wa serikali, wawekezaji na mashirika yanayotaka ardhi na rasilimali za watu wa asili hutawala na kudhibiti mchakato wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.



Kikao cha wanajamii wa asili cha kuandaa rasimu yao ya itifaki kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

Kwa ajili ya kukabiliana na ushawishi wa watu kutoka nje katika kudhibiti upatikanaji wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa Na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, mara kwa mara Watu wa Asili huandaa itifaki zao wenyewe kuhusu haki hizo kwa lengo la kuwaongoza wanapokuwa kwenye majadiliano na wawekezaji na maofisa wa serikali. Kwa kuweka wazi kanuni za kufuatwa na wawekezaji na maofisa wa serikali wanaotafuta ardhi na rasilimali, itifaki hizi husaidia kushughulikia ukosefu wa usawa wa kimamlaka na taarifa, kuimarisha uwezo wa kujitawala, ulinzi wa maeneo, na haki za kitamaduni. Itifaki hizo zinakabiliana na hati za kisheria zinazotambua rasmi kuwa Watu wa Asili wana sheria zao na utaratibu wanaotamani kuwa nao wa kupigania majadiliano na serikali na wawekezaji kwa ajili ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

Muda wote, Watu wa Asili daima wamekuwa na itifaki zinazosimamia ushirikishwaji na watu kutoka nje ya jamii yao, ikiwemo itifaki tata, zenye maoni tofauti kuhusu ama watu wengine wanaweza kutumia ardhi, rasilimali na maeneo yao, ama la. Mara nyingi kanuni hizi ni sehemu ya mapokeo na mifumo isiyoandikwa na zilikuwa na nguvu katika kusimamia masuala ya kiutawala na maingiliano kati ya Watu wa Asili na watu wengine wa kutoka nje. Itifaki zilizoandikwa za Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi ni mfumo mpya wa kuandika sheria zinazohusu Watu wa Asili.

Itifaki hizo mpya zilizoandikwa za kupigania Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi zilizo nyingi zimekubalika na mahakama za nchi husika pamoja na mamlaka za kieneo, kitaifa, kikanda na kimataifa (*Tazama kisanduku ukurasa wa 14*). Hii inamaanisha kuwa Watu wa Asili wanayo haki ya kuamua namna ya kufanya majadiliano kuhusu haki hizo. Kadiri Watu wa Asili wanavyoandaa itifaki za haki zao za Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi – na zinatambulika na mahakama kama haki halali – uwezo na mamlaka ya kisheria ya itifaki hizo unaongezeka. Kadiri Jamii za Asili zinavyozitaka serikali na wawekezaji kuzingatia itifaki zao zinazohusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, ndivyo itakavyowezekana kuwa "utaratibu huu' mpya utaibuka ambao unaweka mkazo katika sheria za Jamii za Asili na kuwa msingi wa kutetea haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. **Sehemu ya 2** inaongelea namna ya kuandika itifaki ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi na mambo ya kujumuishwa.

## WAKATI MAJADILIANO KUHUSU HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI HAYAFANIKISHI KUPATA HAKI HIZO

**Uzoefu unaonesha kuwa majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi mara nyingi yanakuwa na ukosefu wa usawa wa mamlaka na kunyimwa kwa taarifa.** Kiuhalisia hii inamaanisha kuwa:

- **Wawekezaji na/au maofisa wa serikali wanaweza kufanya "mashauriano" kama fursa ya kufahamisha jamii kuwa kutakuwepo na mradi wa uwekezaji au maendeleo**. Wawekezaji wanaweza kufika kwa mara ya kwanza wakisindikizwa na maofisa wa serikali wanaoiambia jamii kwamba "wanashirikishwa" na kuombwa wakubali mara moja. Katika hali kama hizi, waendelezaji wa mradi hawatoi muda kwa jamii ya Watu wa Asili kuujadili mradi wao wenyewe peke yao, kutafuta ushauri huru, kukusanya taarifa, na kisha kufanya uamuzi, wakiwa peke yao na kulingana na taratibu zao.
- **Wawekezaji na maofisa wa serikali wanaweza kushinikiza au kulazimisha jamii ya Asili kuridhia.** Wanajamii wanaoomba maelezo zaidi, kudai mawasiliano kimaandishi, au kuuliza kuhusu tathmini ya athari za kimazingira au kijamii wanaweza kukumbana na matishio na mateso yaliyoratibiwa na Serikali. Katika hali kama hizi, jamii inaweza kuhisi kulazimishwa, kushinikizwa, au kutishwa, au kwamba hawana chaguo ila kuukubali mradi ambao tayari umeidhinishwa na serikali yao. Katika hali mbaya zaidi, jamii zinazochagua kupinga mradi unaopendekezwa zinaweza kukabiliwa na vitisho au ukatili, kubambikizwa kesi, na kukamatwa kwa makosa ya uwongo na serikali au mwekezaji na mawakala wake.
- **Serikali na/au wawekezaji wanaweza kushinikiza jamii kuikubali miradi ambayo hawaielewi kwa ukamilifu.** Wakati mwingine, wawekezaji au maofisa wa serikali hawatoi taarifa mpaka walazimishwe na jamii. Wawekezaji au maofisa wa serikali hawawezi kuwapa wanajamii taarifa kamili kuhusu shughuli za mradi; faida itakayopatikana kwa mwaka; athari za mradi kwa maji, anga, misitu, udongo, maeneo ya ibada, na afya ya jamii na mfumo wa ikolojia; na mambo mengine muhimu. Hata kama taarifa hizo zitatolewa, hazitakuwa katika lugha au muundo ambao jamii zinaweza kuelewa. Wawekezaji na maofisa wa serikali wanaweza pia kuwalazimisha wanajamii kutia saini mikataba kabla ya kupata fursa ya kuuliza maswali, kuupinga mradi, kuomba vipengele vya miradi vibadilishwe ili kupunguza uharibifu katika jamii au mfumo wa ikolojia, au hata kukataa kabisa mradi huo.
- **Maofisa wa serikali au wawekezaji wanaweza kuomba tu ridhaa ya baadhi ya wanajamii** au wanaweza kufanya ufisadi kwa kuwahonga viongozi ili watie saini fomu za idhini. Wanaweza kuwaondoa madarakani viongozi wa kijamii wanaopinga uwekezaji na kuwaweka watu wao "wanaoelekea" kupendelea maslahi ya watu wa nje.
- Maofisa wa serikali au wawekezaji **wanaweza pia kujaribu kuanzisha michakato yao ya kufanya maamuzi** bila ya kuhusisha vyombo vya jadi vya kufanya maamuzi au wawakilishi halali wa jamii.
- Waendelezaji wa mradi wanaweza pia **kuwafanya watu wasiaminiane na kuanzisha migogoro ndani ya jamii** na kati ya jamii zilizoathiriwa, ili jamii hizo zidhoofishwe na migogoro ya ndani.

**Bila ya usimamizi madhubuti wa serikali na utashi wa kisiasa, waendeshaji wa miradi watasababisha majadiliano ya mara kwa mara yatafanya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi kutokuwa na maana**. "Mashauriano" hayo yanaweza kutumiwa na kampuni na/au serikali kuwaonesha watu wa nje, kama vile mashirika ya viwango vya kimataifa au wafadhili, kwamba jamii husika zilipewa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi na hivyo wanajamii hao wameridhia kwa dhati mradi huo.



**Bila ya usimamizi madhubuti wa serikali na utashi wa kisiasa, waendeshaji wa miradi watasababisha majadiliano ya mara kwa mara yatafanya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi kutokuwa na maana.**




Majadiliano ya kilaghai kuhusu Ridhaa ambayo wawekezaji wanawatisha viongozi na wanajamii na hivyo hakuna Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

## MIFANO YA SHERIA NA TARATIBU ZINAZOTAMBUA ITIFAKI ZA HAKI YA WATU WA ASILI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

**Katika ngazi ya kimataifa:**

Mkataba wa Bayoanuwai (CBD) wa Nagoya juu ya upatikanaji na ugawanaji wa faida unarejelea jukumu la itifaki za jamii na haja ya kuongeza ufahamu kuhusiana na itifaki hizo; Umoja wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira (IUCN) umeunga mkono uandaaji wa itifaki za kitamaduni za kibayolojia;

- Kati ya mwaka 2015 na 2017, Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kibinadamu nchini Kolombia ilitoa msaada wa kitaalamu kwa Watu wa Asili wanne katika uundaji wa itifaki.
- Mwaka 2018, Wataalamu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wa Asili walibainisha kuwa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi ni msingi wa kujenga imani katika majadiliano.

**Katika ngazi ya kitaifa:**

- Mwaka 2016, Jaji wa Argentina alitoa amri ya kutambua itifaki ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi kwa jamii 33 za Kollo na Atacama katika eneo la Salinas Grandes y Laguna de Guayatayoc na kutoa wito kwa wizara zote na taasisi za serikali kuzitambua itifaki za jamii hizo.
- Mwaka 2006, Mahakama ya juu ya Ontario, Canada ilitambua itifaki za Kitchenuhmaykoosib Inninuwug (KI).
- Mwaka 2011, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa lilishirikiana na Shirikisho la Jamii za Asili zinazopigania Kujitambua nchini Paraguay katika kuandaa itifaki ya kitaifa ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, ambayo baadaye ilitambuliwa rasmi na tamko la Rais mwezi Desemba mwaka 2018; na
- Mwaka 2016, Mahakama ya Kikatiba ya Colombia iliamuru kuwa itifaki ya jamii ya watu wa Embera Chamí ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi lazima iheshimiwe.
- Mwaka 2018, Mahakama ya Juu ya Brazil iliamuru kuwa majadiliano yajayo ya watu wa jamii ya Juruna yaheshimu haki yao ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

**Chanzo:** *A Whitmore & H Tugendhat (2019) (eds), Free Prior Informed Consent Protocols as Instruments of Autonomy: Laying Foundations for Rights based Engagement (Infoe, ENIP) at pp. 19-21. Available at: https://enip.eu/FPIC.pdf*

**Endapo majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi yakiongozwa na Jamii za Asili kwa mujibu wa vigezo walivyoweka wenyewe kwa ajili ya kulinda haki zao.**

# KUJIANDAA: KABLA YA MAJADILIANO KUANZA 02



Uwekaji wa alama za ardhi za jamii ya watu wa asili na kuainisha bayoanuai inayopatikana kwenye eneo husika.

**Ni muhimu kujiandaa vema kwa ajili ya majadiliano ya baadaye kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.** Sehemu hii ya mwongozo inaeleza kuhusu masuala ambayo jamii yenu inaweza kujiandaa nayo mapema kwa ajili ya majadiliano kuhusiana na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Ni vema kutenga muda wa kutosha kwa ajili ya kuzifahamu haki zenu za kisheria, na kuandaa rasimu yenu ya itifaki za haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, kuweka mpango wa namna ya kushughulikia mawazo kinzani ndani ya jamii, na kueleza dira yenu kwa ajili ya mustakabali wa jamii yenu, na hilo litawasaidia kuijenga jamii imara na itakayokuwa imejiandaa vizuri kwa ujio wa wawekezaji wanaokuja kutaka rasilimali zenu.

**Ikiwa jamii yenu haijaandika mwongozo kuhusu haki ya kujulishwa, kuelewa na kukubali kwa hiyari kabla ya kufanya maamuzi na mnafuatwa na wawekezaji na/au maofisa wa serikali wakitaka rasilimali zenu,** mnaweza kufuata hatua zilizoelezwa katika sehemu hii mara tu baada ya mwekezaji na/au maofisa wa serikali wanafika kwenye jamii yenu. Mnaweza kuwaomba wawaruhusu mfanye majadiliano ya kwanza kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi ili jamii yenu ipate muda wa kutosha wa kujiandaa, kujipanga, na kuwa tayari.

## MWEKEZAJI ANAPOWASILI, TAFUTENI MSAADA WA KISHERIA NA KIUTAALAMU KWA HARAKA

Mwekezaji anapofika kwenye jamii yenu kwa mara ya kwanza, jitahidini mara moja kujifunza vya kutosha kuhusu mradi uliopendekezwa na kuelewa athari zinazoweza kujitokeza katika maisha yenu na kwa mifumo ikolojia ya eneo lenu. Ikiwezekana, tafuteni msaada wa wataalamu wa sheria na kiufundi wanaoweza kuwasaidia kujua zaidi. Mnaweza kutafuta shirika linaloweza kutoa msaada huo bila malipo, au kwa gharama nafuu sana.

## MSISAINI AU KUKUBALI CHOCHOTE

Msisaini nyaraka zozote kutoka kwa waandaaji wa mradi hadi mtakapothibitisha kuwa mchakato wa kupata haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiari Kabla ya Kufanya Maamuzi umekamilika. Ikitokea mwekezaji anaiomba jamii yenu ikubali jambo fulani au anawapa rasimu ya mkataba muusaini, mwambieni mwekezaji kuwa hamtasaini chochote kama ya jamii yenu kufanya maamuzi. Tambueni kuwa maofisa wa serikali na wawekezaji wakiwa na nia ovu wanaweza kutumia vibaya nyaraka yoyote mliyosaini kama ushahidi wa uwongo kwamba mmeridhia kwa kutumia haki yenu ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi .

## ANDIKENI NA/AU REKODI SAUTI NA VIDEO KILA AINA YA MAZUNGUMZO NA MWANDAAJI WA MRADI

Weka rekodi ya kila mawasiliano mnayofanya na waandaaji wa mradi, yakiwemo ya simu, endapo itawezekana na ni salama kufanya hivyo. Ni vyema kutunza nakala za barua, barua pepe, au ujumbe wowote wa maandishi mnaotuma au kupokea kutoka kwa mwekezaji au serikali. Kutunza maandishi na nyaraka kunaweza kusaidia ikiwa:

1. Kutatokea mkanganyiko au mgogoro kati ya jamii yenu na wasimamizi wa mradi na kushindwa kuelewana;
2. Hamjaridhia mradi na mnapata matatizo ya kulipiziwa kutokana na uamuzi wenu;
3. Mnaridhia mradi na baadaye mwekezaji na serikali wanakiuka mkataba mliokubaliana;
4. Mradi unaharibu maeneo yenu ya matambiko, kuchafua mazingira, kukiuka haki za binadamu, au kuiathiri jamii yenu; na/au
5. Mradi unawazuia wanajamii kutumia msitu, ardhi, maji na rasilimali nyingine zinazotegemewa na jamii yenu kwa ustawi wake, na athari nyingine hasi za mradi.

Katika mojawapo ya matukio haya, mkiamua kuwapeleka wawekezaji mahakamani, kama mlitunza kumbukumbu za mawasiliano yote na maandishi basi vitakuwa ushahidi wa kusaidia katika kesi yenu.

# MJIANDAE WENYEWE KWANZA

## 1. Teteeni vipaumbele vya jamii yenu

Inaweza kusaidia endapo mtakuwa na sauti moja kama jamii na kuafikiana kuhusu vipengele fulani vya msingi vya namna mtakavyoipokea miradi au uwekezaji wa siku zijazo utakaoanzisha majadiliano kuhusu haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Baadhi ya mambo mnayoweza kujadili ni pamoja na:

- Je! jamii yenu ina maono gani ya kustawisha mustakabali wenu? Dira hii inaweza kuwa kipaumbele katika majadiliano na mazungumzo yenu yote na wawekezaji na maofisa wa serikali wanaotafuta rasilimali. (Angalia Kiambatisho D kwa ajili ya mwongozo wa kupata dira sahihi kwa siku zijazo.)
- Je, mko tayari kumruhusu mwekezaji kutumia ardhi yenu? Kuna uwezekano kwamba wanajamii watagawanyika kuhusu hili, huku baadhi yenu wakiwa na shauku ya kupata kazi na fursa zinazoweza kuja na uwekezaji huo, na wengine wakipinga vikali uwekezaji. Itafaa kama mtajadili swali hili ili kila mtu aweze kuelewa maoni mbalimbali ya jamii ajili ya kuhakikisha kuna haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.
- Iwapo mko tayari kuruhusu uwekezaji, ni “mambo gani ya jamii yenu yasiyojadilika?” Mambo hayo yanaweza kuwa, kwa mfano, maeneo ya kijiografia ambayo ni marufuku kwa watu wa nje (kama vile maeneo ya matambiko, maeneo ya mazishi, maeneo ya kiakiolojia au ya kihistoria, maeneo ambayo yenye mimea iliyo hatarini kupotea, maeneo muhimu ya maji, ardhi ya kilimo, nk). Mambo hayo yasiyojadilika yanaweza pia kuwa kupiga marufuku teknolojia fulani au shughuli za uziduaji.
- Je, ni aina gani ya miradi inayoweza kuwanufaisha bila ya madhara makubwa, na ni aina gani ya miradi mtaikataa moja kwa moja kwa hoja ya kuwa na madhara makubwa?

## 2. Imarisheni mshikamano wa jamii, toeni nafasi kwa mawazo mbalimbali, na hakikisheni mnaweka mifumo mizuri ya utatuzi wa migogoro

Mshikamano wa kijamii — kuwepo kwa hisia ya kuwa wamoja na wenye tunu zinazofanana miongoni mwa wanajamii — ni jambo muhimu kwa ajili ya maamuzi shirikishi, ya amani na yenye ufanisi kuhusu masuala ya matumizi na usimamizi wa ardhi na rasilimali. Bila ya umoja wa kijamii, itakuwa vigumu kwa jamii yenu kuwa na mijadala inayohusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, kuamua kuridhia au kutoridhia, na kujadili mikataba yoyote baada ya kuridhia.

Kuimarisha mshikamano wa jamii yenu pia kutasaidia kuzuia ghiliba za wawekezaji na maofisa wa serikali wanaowalaghai kwa kusababisha kuwepo na kutoelewana na mifarakano ndani ya jamii ya watu wa asili, kunufaika na migawanyiko ndani ya jamii, au kujaribu “kuwagawanya na kuwashinda” kwa ajili ya kuhakikisha wanapata ridhaa ya wanajamii. Jamii ambazo ziko wazi kwenye mifumo yao ya utawala na zimekuza mshikamano kati yao ziko imara zaidi kukabiliana na mbinu kama hizo za kuwagawanya na kushinda. Jamii itafute mikakati itakayowasaidia mbaki mmeshikamana wakati wa mazungumzo na majadiliano na wawekezaji.

Itakuwa jambo la maana kupanga namna ya kushughulikia tofauti za mawazo na kusimamia migogoro wakati wa mijadala inayohusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.  Wanajamii wanaweza kuwa na maoni tofauti kuhusu mradi uliopendekezwa, na migogoro ya ndani inaweza kutokea. Jamii yenu iwe tayari na mfumo madhubuti wa kitamaduni wa kushughulikia migogoro; la sivyo, mnaweza kuandaa mpango wa utatuzi wa migogoro ili kudhibiti kutoelewana miongoni mwa wanajamii.

Mnaweza pia **kuandaa utaratibu wa mawasiliano ambao utahakikisha kuwa taarifa za mradi zinatolewa kwa jamii nzima kwa njia zenye ufanisi na za uwazi**. Ni muhimu kuhakikisha kuwa mchakato wa kufanya maamuzi haupotoshwi na wasomi wa kwenye jamii, wanasiasa, au na “kikundi kidogo” cha watu ndani ya jamii kubwa sana. Iwapo jamii yenu haina desturi za kijadi za upashanaji taarifa, inaweza kutengeneza mfumo utakaohakikisha wanajamii wote wanashiriki kikamilifu katika mikutano muhimu kwa ajili ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

## SHIRIKISHA JAMII NZIMA

**Michakato ya kufanya maamuzi ambayo ni ya uwazi na ya pamoja hutoa nafasi ya ushiriki sawa wa wanajamii wote kulingana na mifumo yenu ya kitamaduni ya kupangilia mambo. Hilo likifanyika litasaidia jamii yenu kufanya maamuzi bora kuhusu itifaki za Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.** Kwa mfano, watu wengine wanaweza kujua mahali zilipo dawa na vyakula fulani ambavyo wengine hawajui, na wengine wanaweza kujua kuhusu sehemu fulani muhimu za ufugaji, uwindaji au uvuvi ambazo wengine hawajui. Vile vile, viongozi wa kiroho wanaweza kuonesha alama kwenye mipaka ya maeneo ya siri kwa ajili ya matambiko. Bila ushiriki wa kila mtu, jamii yenu inaweza kuridhia mradi wa uwekezaji ambao utaathiri sehemu fulani ya jamii. Ingawa jamii yenu inaweza kuwa na njia zake za kitamaduni za kuhakikisha kwamba kila mtu anashirika katika maamuzi muhimu, bado ni vizuri kuwa na mifumo itakayohakikisha kwamba kila mtu ana sauti katika kujadili masuala ya haki ya kujulishwa, kuelewa na kukubali kwa hiyari kabla ya kufanya maamuzi.

Mnaweza pia kufikiria jinsi mnavyoweza kushirikiana na kuratibu kwa pamoja na jamii jirani. Mara nyingi, jamii kadhaa, za Watu wa Asili na wasio wa asili, huathiriwa na mradi mmoja. Wasimamizi wa mradi wanaweza kujadiliana na makundi mbalimbali kwa nyakati tofauti kama njia ya kuwagawa na kuwashinda. Kushirikiana na kupeana taarifa kunaweza kuleta matokeo bora kwa makundi yote yaliyoathiriwa.



## 3. Fafanua mipaka ya ardhi yenu na weka alama kwenye maeneo maalumu yaliyotengwa kwa matumizi ya kijamii

Itafaa endapo jamii yenu itahakikisha mipaka ya eneo lenu iko wazi. Mnaweza pia kuangalia ramani ya ardhi yenu na muweke alama kwa maeneo yaliyotengwa kwa matumizi ya jamii, kama vile vyanzo muhimu vya maji kwa ajili ya uhakika wa upatikanaji wa maji kwa sasa na kwa baadaye; ardhi ya kilimo, misitu, au maeneo ya malisho ambayo ni muhimu kwa ajili ya uhakika wenu wa chakula; maeneo kwa ajili ya matambiko na maziko ambayo ni muhimu kwa uhusiano wenu wa kiroho na ardhi yenu; na maeneo ya makazi na masoko. Ikiwa jamii yenu iko tayari kuridhia mradi wa uwekezaji, weka mipaka ya ardhi ambayo hamko tayari kukodisha kwa mwekezaji na bainisha sehemu ya ardhi itakayobaki chini ya udhibiti wa jamii yenu.

**Kila Jamii ya sili ina mfumo wake wa kufanya maamuzi na mfumo wake wa mila na desturi. Majadiliano yenu kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi yanaweza kutokana na mfumo wa toka huko nyuma wa kimila, na maamuzi mnayofanya yanaweza kuzingatia mfumo huo uliozoeleka.**

## 4. Zifahamu haki zenu za kisheria kuhusu ardhi na mifumo ya ikolojia kwa mujibu wa sheria za nchi

Ni muhimu kujua haki zenu rasmi za ardhi zilizo ndani ya mfumo wa kisheria wa nchi ambapo ardhi au eneo lipo, kwani haki hizo zinaweza kuathiri namna serikali inavyoshughulikia haki yenu ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanywa Maamuzi. Fanya kazi kwa karibu na mwanasheria, au wakili ili kujua haki zenu kisheria. Angalia hasa sheria ya mazingira ya nchi yako, sheria ya misitu, sheria ya maji, sheria ya rasilimali za ardhi na chini ya ardhi, sheria ya mikataba, sheria ya uwekezaji, na sheria ya umilikishwaji ardhi. Tazama Kiambatisho E kuelewa makundi ya wataalamu wanaoweza kuwaunganisha na mashirika ya kitaifa na kimataifa yanayotoa huduma hizi.

Ni vema pia kuelewa taratibu za serikali za kuidhinisha miradi ya uwekezaji, ikijumuisha mikutano yoyote ya hadhara inayohitajika; aina za vibali na leseni ambazo mwekezaji anapaswa kupewa na serikali; na masharti mengine ambayo mara nyingi serikali huweka kwenye miradi ya uwekezaji. Kuzielewa taratibu hizi kutawasaidia kuishawishi serikali wakati wa mchakato wa kuidhinisha mradi, na/au kujiridhisha kama mwekezaji amefuata taratibu za serikali na ana haki kisheria ya kuendesha mradi.

Pia, baadhi ya nchi zina sheria na sera zinazodhibiti uwekezaji wa kampuni za kigeni zilizosajiliwa ndani ya nchi. Ikiwa mradi unaendelezwa na mwekezaji wa kigeni, mnaweza kujiridhisha kwenye sheria zinazosimamia mashirika katika nchi husika. Sheria hizo zinaweza kusaidia kuondoa madhara na kulazimisha mwenendo mwema wa wawekezaji wa kigeni.



Wanajamii wakijifunza kuhusu haki zao za kisheria za Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

## 5. Jifunze namna wawekezaji na maofi sa wa serikali wanavyothaminisha ardhi na rasilimali zenu

Mnaweza kutafiti kuhusu hali ya soko la ardhi mijini na vijijini nchini mwenu ili kujua thamani ya kuuza au kukodisha ardhi kwenye soko. Ikiwa mradi unaopendekezwa unahusisha uvunaji wa rasilimali zilizomo katika ardhi yenu, mnaweza pia kutafiti kwenye masoko ya kitaifa na kimataifa kuhusiana na thamani ya rasilimali hizi (Kwa mfano, ikiwa ni mradi wa kukata magogo, mnaweza kutafiti thamani ya mbao kwenye masoko ya kimataifa).

Inafaa pia kuelewa thamani ya ardhi na rasilimali zenu kwenu ninyi wenyewe ili mnapojadiliana na wawekezaji na maofisa wa serikali mnaongea kwa uwazi. Ardhi ya kawaida kama vile ya malisho, misitu, na ardhi oevu huwa ya thamani kubwa kwa jamii za watu wa asili. Hata hivyo, kwa wanajamii waliozoea kupata mahitaji yao ya nyumbani kama vile kuni, mimea dawa, na matunda na mboga za porini kutoka katika maeneo hayo, inakuwa vigumu kuthamanisha vitu hivyo. Ikiwa jamii haijui thamani ya hivi vitu, mnaweza kujikuta mnakodisha ardhi yenu kwa wawekezaji kwa bei ya chini sana kuliko thamani halisi iliyo nayo kwa sasa. Ingawa siyo rahisi kupata thamani ya rasilimali fulani (kama vile maeneo ya matambiko na kuzikia n.k.), rasilimali nyingine kama kuni za kupikia zinaweza kuthaminishwa kwa urahisi zaidi. Tazama Kiambatisho C kuona namna ya kukokotoa thamani ya rasilimali za kwenye ardhi yenu ya pamoja. Jamii ambazo zimekamilisha zoezi hili kwa kawaida hupata zaidi ya dola za Kimarekani milioni 1 kila mwaka. Baada ya kukokotoa thamani ya ardhi na rasilimali zenu, mnaweza kutumia thamani hiyo katika majadiliano na mazungumzo na wawekezaji na maofisa wa serikali.

# PAZA SAUTI YENU KUHUSU HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

Kama ilivyoelezewa katika **Sehemu ya kwanza,** Watu wa Asili wamekuwa wakiandika miongozo kuhusu haki zao za Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, ili wakati mwekezaji yoyote anakuja kuomba ardhi na rasilimali kwa ajili ya kuwekeza, basi mchakato akute tayari wanao mwongozo wa kusimamia majadiliano na wanasimamia vizuri haki yao ya kutaka Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Ni jambo jema kuwa na mwongozo utakaowasimamia kuhusu yaki yenu ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, na mwongozo huo utaelekeza namna jamii yenu itashauriana na kuhakikisha kuwa mnatetea haki zenu. Sehemu ifuatayo inajikita katika uchambuzi wa miongozo ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi iliyoandikwa na Watu wa Asili, pamoja na mifumo bora iliyopo kwa sasa. Mwongozo wenu wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi utahusisha:

## 1. Utangulizi unaoelezea historia ya jamii yenu na kwa nini mmeamua kuandaa mwongozo wenu

Sehemu hii inaweza kuwa na:

- Historia yenu kama Watu wa Asili;
- Mfungamano wenu na ardhi na maeneo yenu ya kihistoria, kitamaduni, kiroho, na masuala ya ustawi;
- Mitazamo yenu kuhusu maisha, maadili, imani, na kosmolojia;
- Mahusiano na mfungamano yenu na ardhi na rasilimali;
- Maelezo kuhusu mfumo wenu wa kijadi wa kupanga na kufanya maamuzi (na umuhimu wa kufanya maamuzi kwa pamoja katika utamaduni wenu, kama upo);
- Maono yenu ya ya kuifanya jamii yenu ya baadaye yenye kustawi;
- Maelezo ya namna maisha yenu ya kijadi yanavyofungamanishwa na ardhi yenu na mifumo kiikolojia;
- Maelezo ya kina kuhusu ardhi au eneo lenu na hati miliki au hati rasmi za ardhi hiyo; na
- Taarifa nyingine muhimu zinazoelezea sababu ya kuwa na mwongozo wenu.

## 2. Ni miradi ipi hamtaikubali

Katika mwongozo wenu mnaweza kubainisha shughuli kadhaa ambazo hamtaridhia kufanyika katika eneo lenu. Kwa mfano, mnaweza kukataa kuruhusu miradi mikubwa ya kufua umeme wa maji ambayo itaharibu vyanzo vyenu maji, kukausha vyanzo vya maji, na kuathiri upatikanaji wa uhakika wa maji.

- Ni vyema kueleza sababu za kuzikataa shughuli hizi, mkieleza uamuzi wenu kwa ushahidi wa jinsi miradi kama hiyo itakavyotishia uhai na kuathiri ustawi wa jamii yenu, uhakika wa chakula na maji, au kuathiri taratibu zenu za matambiko.
- Ikiwa mnaorodhesha shughuli zilizopigwa marufuku katika mwongozo wenu, mnaweza kusema kwa uwazi kwamba ingawa hamkatai majadiliano, lakini kuhusu hayo mmeshafanya uamuzi kuhusiana na mradi huo, na kwamba uamuzi wenu wa kukataa kuridhia umefanywa na umeandikwa rasmi
  (Msimamo huu unaendana na hoja ya kisheria kwamba majadiliano ni haki, na siyo wajibu, kwa Watu wa Asili.)
- Mnaweza pia kutangaza kwamba uhamishaji na uondoaji wa makazi haukubaliki na kwamba mradi wowote unaolazimisha watu kuhama makazi utasababisha kukosa ridhaa yenu.

## 3. Masharti ya kuwa na majadiliano yenye tija

Mwongozo wenu unaweza kuweka vifungu muhimu vya majadiliano kuhusu haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, vikiwemo:

- Kwamba pande zote zinazohusika zitambue ardhi, maeneo, na rasilimali zenu kama mnavyozitambua ninyi, hata kama hamna hati miliki;
- Kwamba Serikali na maofisa wake lazima watambue, waheshimu, na kulinda haki zenu za kisheria chini ya sheria za kimataifa na kitaifa;
- Kwamba Serikali na maofisa wake wote lazima watambue mfumo wenu wa utawala wa kijadi, ukijumuisha miundo na taasisi zenu pamoja na mfumo wa kisheria wa Watu wa Asili; na
- Kwamba Serikali na maofisa wake wote lazima wawapeni maarifa sawa kama wanavyopewa watu wasio wa asili wakati wote wa majadiliano.

## 4. Kanuni za maadili zinazohusu miongozo ya kitamaduni

Mwongozo wenu unaweza kueleza namna mnavyoheshimiana na kusikilizana wakati wa majadiliano.

## 5. Mambo yatakayoharibu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi na kuufanya mchakato wa kupata ridhaa kuwa batili

Mwongozo wenu uorodheshe mambo ambayo yatabatilisha mara moja majadiliano kwa ajili ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, yakiwemo:

- Ukatili, vitisho, udhalilishaji, au vitisho;
- Kukamatwa, kuteswa, kuwepo kwa makundi yenye silaha wakati wa mashauriano, na serikali kutumia nguvu;
- Rushwa, kutoa zawadi kwa viongozi na baadhi ya wanajamii, na jitihada nyingine za kifisadi za kushawishi maamuzi;
- Kuanzisha kwa makusudi mipasuko ndani ya jamii au kati ya jamii na jamii;
- Kushindwa kutoa taarifa muhimu kuhusu mradi kwa kujua, kwa nia ovu;
- Kughushi saini au uthibitisho wa ridhaa na hatua zingine za kilaghai zinazoweza kufanywa na wawekezaji na maofisa wa serikali; na
- Kukataa kutambua kuwa mnayo haki ya kutoridhia.

## • 6. Majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa Na Kukubali kwa Hiyari Kabla Ya Kufanya Maamuzi yafanyike kabla ya serikali kufanya maamuzi

Kwa sababu serikali nyingi huwa zinaanzisha mchakato wa kuwepo kwa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi baada ya maofisa wa serikali kutoa leseni au vibali au baada ya kusaini mikataba na wawekezaji, mwongozo wenu unatakiwa kueleza bayana kuwa majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi lazima yafanyike:

- Kabla serikali haijatoa leseni au vibali vyovyote;
- Kabla ya kuanza maandalizi ya mradi;
- Kabla ya kusainiwa kwa mkataba kati ya serikali na mwekezaji;
- Kabla ya kuanza kupanga na kutekeleza mradi;
- Kabla ya kufanyika kwa tathmini ya athari; na
- Kabla ya hatua yoyote mpya inayohusu mradi au maendeleo yoyote makubwa mapya ya mradi ambao jamii yenu imeuridhia.

## 7. Ratiba na hatua za majadiliano kwa ajili ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi

Mwongozo wenu kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi unaweza kutakiwa kuzingatia michakato ya kufanya maamuzi ya ndani ya jamii na kuwa vipindi virefu na vingi vya mikutano ya pamoja, ili jamii yenu ipate muda wa kutosha wa kuuelewa mradi na kuamua kuhusu majibu yenu. Mwongozo wenu pia unapaswa kueleza hatua mbalimbali za kufikia viwango vya majadiliano kuhusu mwongozo kwa ajili ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

## 8. Mpangilio wa uandaaji wa mikutano yakujadili Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi

Mwongozo wenu unaweza ukaeleza mpangilio mbalimbali wa namna ya kukutana, ikiwemo:

- **Mahali pa kukutania: Mikutano yote itafanywa katika eneo lenu.** Ni vyema liwepo eneo la mkutano linalofikika kirahisi na watu wote na majadiliano yafanyike katika eneo ambalo kila mtu atajisikia vizuri. Ikiwezekana, ni vema mkikutana eneo la wazi ili watu wote washiriki.
- **Lugha ya mkutano: Mikutano yote itafanywa kwa lugha yenu wenyewe, na ukalimani ufanywe kwa wasiozungumza lugha yenu (*siyo ninyi kufanyiwa ukalimani*).** Wanajamii wenu lazima waelewe na kuwasiliana kwa uhuru katika mijadala yote inayohusu haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Mikutano ifanyike kwa lugha yenu na wakalimani wawepo kwa ajili ya wawekezaji na maofisa wa serikali.
- **Wanaoweza kushiriki mikutano:** Mnaweza kuwa na uhuru wa kuamua kama jamii kuwaalika watu wengine kama vile waandishi wa habari, wanasheria, wataalamu, na mawakili nk kuja kushiriki kwenye mikutano, na kueleza ni wawakilishi gani wa kampuni mnashughulika nao, vilevile ni maofisa wangapi wa serikali wanaweza kushiriki.
- **Namna ya kupata pesa kwa ajili ya kugharimia vikao vyote vya majadiliano kuhusiana na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi:** Mchakato wa kujadili haki hii unahitaji kuwa na vikao vingi, huduma za ukalimani na tafsiri, na kuchapisha nyaraka, vyote hivyo vinahitaji pesa. Katika mazingira mengi,wekezaji anatakiwa kulipia gharama zote; na mwongozo wenu unatakiwa kueleza hivyo.

Jamii yenu lazima ieleze kuwa mwongozo wenu unatakiwa kuhakikisha kuwa uamuzi wa kugharimia mikutano yote usiathiri au kutumika kushawishi mchakato wa kujadili Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

- **Uratibu na upangaji wa mikutano**: nani ataratibu michakato hii, na nani ataongoza mikutano**.**
- **Kuweka kumbukumbu na kurekodi:** Ni vema vyote viwili vikifanywa na mtu anayeaminika asiyeegemea upande wowote na mwanajamii.
- **Maelezo mengine yoyote ambayo jamii inaona ni ya muhimu.**

## 9. Ni taarifa zipi mtazihitaji kwa ajili ya kupata ufahamu zaidi, na namna gani mtazipata taarifa hizo

Mwongozo wenu unaweza kutaja taarifa za mdomo na za maandishi mnazohitaji, ambazo zitatafsiriwa kwa usahihi katika lugha yenu ya asili. ***Tazama hapo chini*** kwa maelezo zaidi kuhusu taarifa mnazohitaji kuzipata.

## 10. Mchakato wa kuamua ama kuridhia au kutoridhia-na hatua za kufuata kuhakikisha kuwa watu wengi wameshirikishwa

Mwongozo wenu wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi unaweza kuwa na maelezo ya namna jamii yenu itafanya maamuzi ya kuridhia au kutoridhia, ikiwemo mikakati ya kuhakikisha watu wengi kwenye jamii yenu wameshirikishwa katika maamuzi hayo.

**Ridhaa ya Watu wa Asili lazima ipatikane kabla ya kuanza kwa shughuli za mradi, hatua ya maandalizi ya mradi; kabla serikali haijatoa leseni au vibali vyovyote, kabla ya kuanza utafutaji wa sehemu ya kuanzisha mradi, na kabla ya serikali kusaini mkataba na mwekezaji.**

**Mwongozo wenu unaweza:**

- Kuwafanya mfanye maamuzi kulingana na michakato yenu ya jadi;
- Kuufanya mchakato kuwashirikisha wanajamii wote katika kufanya maamuzi, badala ya viongozi peke yao;
- Kuhakikisha kuwa mijadala yote inayohusu haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi inakuwa shirikishi na jumuishi, na kwamba wanawake, vijana, wanaume, wazee, na watendaji wa sekta nyingine za maisha, wote washiriki katika mchakato wa mwisho wa kufanya maamuzi; na
- Kusaidia kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa maoni ya kila mtu yamezingatiwa.

## 11. Hatua ambazo mwekezaji na serikali wanapaswa kuchukua ikitokea mradi unawaathiri Watu wa Asili kwa wingi

Mwongozo wenu unaweza kueleza namna majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi yanapaswa kuendelea baada ya kuona makundi mbalimbali yameathiriwa na mradi. Kwa mfano, kama mradi utaathiri mandhari kubwa kama vile safu ya milima au vyanzo vya maji, Watu mbalimbali wa Asili wanaweza kuathiriwa. Vile vile, bwawa linaweza kuathiri makundi mengi ya watu wanaotumia mto huo mmoja. Mwongozo wenu unaweza:

- Kudai haki yenu ya kujipanga kama kikundi;
- Kumzuia mwekezaji kuendelea na mikakati yake ya "kuwagawanya na kuwashinda";
- Kueleza namna mtakavyoshirikiana na kufanya maamuzi kama kikundi;
- Kuweka mikakati ya kushughulikia migawanyiko ndani ya kikundi au kati ya jamii moja na nyingine; na
- Kubainisha masuala mengine yoyote ya kiuratibu ndani ya jamii.

**Hii orodha ya mambo ya kuweka kwenye mwongozo wenu wa majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi ni mapendekezo tu.**

## MASHAURIANO YA AWALI NDIYO NINI? JE YANATAMBULIKA NA SHERIAZA KIMATAIFA?

**Hakuna kitu kinachoitwa "mashauriano ya awali".** Baadhi hauriano ya ya wawekezaji na serikali ,lmujibu wa tamaduni, maslahi na malengo yenu. hutumia neno "mas awali" kama njia ya kuonesha kuwa majadiliano yalifanyika kwa ajili ya kuwapa watu haki ya kujulishwa, kuelewa na kukubali mambo mengine mnayoona ni ya muhimu kuwekwa

kwa hiyari kabla ya kufanya maamuzi. Dhana hii haipo kabisa kwenye sheria za kimataifa. Kufafanua na kuamua jinsi mchakato wa kujadili masuala ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kuamua kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi ni hatua ya kwanza. Huo si mchakato tofauti. Mwongozo wenu unaweza kueleza bayana kuwa "mashauriano ya awali" hayapo, na kwamba mwongozo wenu umebainisha utaratibu wa mchakato mzima.

# TAFUTENI MSAADA WA SHERIA NA

Mwekezaji au ofisa wa serikali anapofika kwenye jamii yenu kwa ajili ya kutafuta ardhi, ni vyema kutafuta msaada wa kisheria na kiufundi haraka iwezekanavyo. Majadiliano yanayohusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubalia kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi yanaweza kuhusisha taarifa za kisheria na kiufundi ambazo ni ngumu kuelewa na mara nyingi huwa na kukosekana kwa usawa wa mamlaka; serikali na wawekezaji mara nyingi wanakuwa na taarifa nyingi zaidi kuliko wanajamii. Mnayo haki ya kupata ushauri huru wa kisheria na kiufundi ili uwasaidie kuelewa zaidi kuhusu mradi uliopendekezwa sawa na watu wengine wanaohusika na mradi huo.

Jumuiya yako inaweza kuuliza wanasheria, wasaidizi wa kisheria, au mawakili wa kisheria kutoa:

- Elimu na mafunzo kuhusu haki zako za kisheria chini ya sheria za kitaifa na kimataifa;
- Ushauri kuhusu masuala changamano ya kisheria;
- Ushauri wa kisheria wakati wa maingiliano na mwekezaji; na
- Uwezo wa kisheria na mamlaka wakati wa mazungumzo.

Muhimu zaidi, ukichagua kutoa kibali chako, wanasheria, wasaidizi wa kisheria, na mawakili wanaweza kukagua rasimu za makubaliano yoyote yanayotolewa ili kuhakikisha kuwa yanalinda jumuiya yako kikamilifu na yatasababisha ustawi na ustawi wa siku zijazo. Wanaweza pia kuhakikisha kwamba makubaliano yameandikwa ipasavyo katika mkataba rasmi ambao unaweza kutekelezeka katika mahakama ya sheria.

Jumuiya yako inaweza kuuliza wataalam wa kiufundi kukusaidia:

- Kufikia na kuelewa nyaraka za mradi, ikiwa ni pamoja na mipango ya biashara, masomo ya mazingira, na tathmini za athari;
- Kuelewa athari zinazowezekana za mradi kiuchumi, mazingira, na kijamii;
- Kubainisha hatari na manufaa ya mradi uliopendekezwa;



Wanajamii wakiwa kwenye kikao na mwanasheria wao, wakiwasilisha matokeo wanayotamani kupata, na kuomba ushauri wa kisheria.

• Kuelewa thamani ya soko la ardhi yenu, faida inayotarajiwa ya kila mwaka ambayo mwekezaji atapata kutokana na mradi huo, thamani ya jumla ya kampuni, na taarifa nyingine za kifedha zitakazowezesha kuwa na makubaliano ya haki kati ya jamii na mwekezaji; na

• Kujadiliana na wawekezaji baada ya kuwa una maarifa ya kutosha na uelewa wa masuala ya kiufundi.

Ni gharama kubwa kuwalipa wanasheria na wataalamu, na kumudu gharama za kuwalipa hawa wataalamu inaweza kuwa changamoto kwa baadhi ya jamii za Watu wa Asili. Iwapo jamii yenu haiwezi kumudu kuwaajiri wanasheria na wataalamu, kuna Mashirika yasiyo ya Kiserikali na mashirika ya kimataifa katika kila nchi ambayo yanaweza kutoa msaada wa kisheria na kiufundi bila malipo.

Vinginevyo, jamii yenu inaweza kuiomba serikali au mwekezaji kutoa usaidizi wa kisheria au kulipia gharama za kuwaajiri wanasheria na wataalamu wengine. Hata hivyo, Iwapo serikali au kampuni itakubali kumlipa mwanasheria au mtaalamu wa kuwasaidia, basi chukueni tahadhari kubwa kwani hilo linaweza kuleta mgongano wa kimaslahi. Mwanasheria anaweza asizingatie maslahi yenu, kwani ataweza kuwa upande wa kampuni. Ukiamua kufuata njia hii, jamii yenu inapaswa kuhakikisha kuwa inayo haki ya kuwachagua na kuwaajiri wanasheria na wataalamu wenu wenyewe; mnaamua yale ambayo mnataka mwanasheria au mtaalamu awasaidie kuyapata; siyo kwamba wakili anawashauri huku amebeba maslahi ya kampuni au serikali; na kwamba pesa zote zinazohitajika kulipia huduma za uwakili au ushauri wa kitaalamu zinatolewa mapema, ili pesa zisiishe kabla hamjapata msaada wowote wa kisheria mnaohitaji.

# JIFUNZE KUHUSU MNYORORO WA UWEKEZAJI WA MRADI MAENEO NYETI

Mara tu unapojua kuwa mradi wa uwekezaji unaweza kuwaathiri, anza utafiti ili kuelewa ni nani anayeufadhili huo mradi. Yajue mashirika, benki, na wawekezaji wa binafsi wanaohusika. Miradi mikubwa kwa kawaida huhusisha mseto wa wadau wakiwemo sekta binafsi na serikali, pamoja na wafanyabiashara, wanaowekeza fedha, na maofisa wanaoiwakilisha serikali au wao wenyewe kama wawekezajiwenza. Mashirika ya kimataifa mara nyingi huunda kampuni tanzu za kitaifa zenye jina tofauti ili kufanya kazi zao katika taifa fulani. Kunaweza kuwa na aina nne tano za kampuni tanzu. Kwa hivyo, inaweza kuwa ngumu kupata taarifa za kina za wanaosimamia mradi. Unaweza kukuta mradi unahusisha kampuni nyingi tofauti katika uwekezaji unaodhibitiwa na sheria tofauti tofauti. Mradi unaweza kuwa na wafadhili mbalimbali, zikiwemo benki za uwekezaji wa kimataifa na mashirika ya misaada ya kimataifa. Itasaidia sana mkiweza kuufahamu mnyororo mzima wa uwekezaji, ikiwemo kampuni mama, kampuni tanzu, na wawekezaji wengine wanaotambulika kisheria, na sheria zinazotumika katika kila moja ya nchi hizo.
Waandaaji wa mradi na waendelezaji wanaweza kuwa:

- Serikali yenu, au mfanyakazi wa serikali mwenye maslahi na uwekezaji (ambaye mara nyingi hulipwa kwa kuwa sehemu ya mradi);
- Serikali ya nchi nyingine;
- Kampuni ya kimataifa;
- Kampuni tanzu ya kitaifa;
- Mamlaka za serikali, kama vile wizara au idara;
- Benki au taasisi za fedha za kimataifa (kama vile Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Asia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, au Shirika la Fedha la Kimataifa); na/au
- Wawekezaji wa kimataifa na wafadhili wa ndani.

Mkishajua ni nani anayeendeleza mradi, mtaweza kubaini anayepaswa kuomba ridhaa yenu na kuamua ni wapi mnaweza kutia shinikizo zaidi kwa ajili ya kuhakikisha kuwa mchakato wa kupata Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi unafuatwa. Kujua mnyororo mzima wa uwekezaji kunaweza kuwasaidia kutambua maeneo nyeti ya mradi mnayopaswa kuyalenga. Katika mnyororo huo wa uwekezaji kutakuwa na taasisi, kampuni, au mtu binafsi anayetaka kulinda heshima yake na ambaye hatataka kujulikana kuwa amekiuka haki za watu wa asili. Iwapo itakuwa vigumu kupata taarifa kuhusu mradi huo, mnaweza kutafuta msaada kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani na nje ya nchi au vyombo vya habari (pamoja na magazeti ya kimataifa na majarida) ambavyo vinaweza kuwa na taarifa kuhusu mradi huo.

# MCHAKATO WA MAJADILIANO

# 03




Viongozi na wanajamii wakiomba taarifa zaidi ili waweze kuwa na ufahamu wa kutosha.

**Iwapo hamjaandika mwongozo wenu wenyewe kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi na wakati huohuo wawekezaji na/au maofisa wa serikali wanakuja kutafuta rasilimali zenu,** mnaweza kufuata taratibu zilizoainishwa katika sehemu hii mara tu mwekezaji na/au maofisa wa serikali wanafika katika jamii yenu. Mnaweza kuomba muitishe mkutano wa kwanza wa mashauriano kuhusu wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi ili jamii yenu ipate muda wa kutosha kujiandaa, kujipanga na kuwa tayari.

## KUJADILIANA SIYO KURIDHIA

Kama jamii ya watu wa asili, mnayo haki ya kujadiliana na wasimamizi wa mradi. Uamuzi wa kuzungumza au kujadiliana na wawekezaji na maofisa wa serikali haimaanishi kuwa mmeuridhia mradi. Mnachokifanya ni kudai haki yenu ya kupata taarifa zaidi kuhusu mradi na kujadiliana ili muweze kuridhia. Mna haki ya kujadiliana kwa wiki kadhaa na kisha mkaamua kuukataa.

Majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi lazima yahakikishe kuwa Watu wa Asili hawashiriki wakiwa na hofu ya matumizi ya nguvu. Katika miradi mingi, makampuni hushirikiana na polisi na wanajeshi "kulinda amani na kuleta utulivu" kwenye maeneo ya shughuli zao. Hii inaweza kuwa ni mbinu ya keleta vitisho, na moja kwa moja ni kuwatishia wanaopinga mradi kwamba watakamatwa au kudhuriwa. Ili kuhakikisha kwamba ridhaa inatolewa kwa uhuru, vikosi vya usalama visivyotakikana havipaswi kuwepo kwenye mikutano au ardhi ya Watu wa Asili wakati wa majadiliano na wakati wa kufanya maamuzi. Katika majadiliano yoyote ambapo watu wa asili wanahisi kutishwa basi hali hiyo inakiuka matakwa ya ya mazungumzo ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi.

Mara tu baada ya jamii yenu na wawekezaji na/au maofisa wa serikali wanaotafuta ardhi na rasilimali kwa ajili ya mradi wa uwekezaji au miundombinu anzeni mazungumzo rasmi kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, na jamii yenu inaweza kuchukua hatua kadhaa, zikiwemo:

1. Kumchagua atakayewawakilisha kwenye majadiliano na maelewano yote yanayohusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi;
2. Kuwasilisha mwongozo wenu kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi kwa wawekezaji na maofisa wa serikali mtakaokutana nao na mkubaliane namna ya kuendelea na mchakato;
3. Kuweka kumbukumbu kimaandishi kuhusiana na mchakato (kuweka ushahidi ambao utahitajika hapo baadaye);
4. Kuhakikisha kuwa mnakuwa na taarifa za kina;
5. Kufanya majadiliano kuhusu mradi unaopendekezwa kwa ajili ya kuepuka hatari na madhara;
6. Kujadiliana kuhusu faida na matokeo chanya ambayo serikali au mwekezaji lazima watoe endapo mtaridhia mradi; na
7. Kufanya maamuzi ya kuridhia au kutoridhia mradi.

Kila hatua iliyotajwa hapa imefafanuliwa katika kurasa za huko mbeleni.

**Kuzungumza au kufanya majadiliano na wawekezaji na maofisa wa serikali haimaanishi mmeridhia mradi. Mnayo haki ya kuendelea kujadiliana kwa wiki kadhaa hadi mfikie uamuzi wa kutoridhia mradi.**

# CHAGUENI WAWAKILISHI WENU KATIKA MAJADILIANO YOTE YANAYOHUSU HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI NA WAANDALIWE VIZURI KWA HILO JUKUMU

Ingawa kwenye jamii yenu kuna viongozi wa kimila au Wazee wanaoheshimika ambao wana nafasi nzuri ya kuzungumza kwa niaba yenu wote, lakini itafaa zaidi kuwa timu maalumu itakayoshiriki katika majadiliano kuhusu "Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi". Na timu hiyo ijumuishe viongozi, wazee wanaoheshimika, wanawake, vijana, na wanajamii wenye ujuzi na maarifa maalumu. Litakuwa jambo jema kama timu hiyo itakuwa na watu wanaoweza:

- Kuwa na msimamo thabiti kutetea masilahi bora ya jamii wakati wa mazungumzo yote, hata katikati ya shinikizo la wawekezaji na/au vitisho;
- Kuwasilisha hoja kwa uwazi na kusikiliza kwa makini (sio tu kwa yale yanayosemwa, lakini kwa yale ambayo hayasemwi);
- Kuoanisha maoni mbalimbali ya wanajamii, maslahi, na wasiwasi wao na kuweka kwenye mkakati wa wazi;
- Kuzielewa ripoti za kiufundi na nyaraka za kisheria;
- Kwa ujasiri kutaka ufafanuzi kukiwa na jambo ambalo haliko wazi;
- Kuchukua vidokezo na video kwa ajili ya kumbukumbu ya yale yaliyojadiliwa na kuamuliwa katika mikutano yote;
- Kutoa taarifa za mara kwa mara zinazohusu mazungumzo hayo na utafute maoni ya ziada;
- Kuhakikisha kwamba wanajamii wanakuwa na mwafaka kamili; na
- Kuandaa mpango wa kudhibiti migogoro ndani ya jamii.

Mnapoamua kuwachagua wawakilishi, mnaweza kujadili maswali yafuatayo:

- Je, wawakilishi wetu wanapaswa kuwa na ujuzi na sifa gani?
- Je,ni majukumu gani kila mjumbe wa timu atakuwa nayo?
- Ni maamuzi gani ambayo timu ya mazungumzo inaweza kufanya? Ni maamuzi gani yanahitaji mwafaka na makubaliano ya jamii nzima?
- Ni mara ngapi, na katika mfumo upi, wawakilishi wanatakiwa kutoa mrejesho wa mara kwa mara kwa jamii, na kutafuta maoni yetu?

**Linaweza kuwa jambo la manufaa ikiwa mtachagua timu maalumu itakayoundwa na viongozi, wazee wanaoheshimika, wanawake, vijana na wanajamii wenye ujuzi mahususi au maarifa fulani ambao watasaidia kusimamia nafasi ya jamii yenu katika majadiliano kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.**

# MKUBALIANE KUHUSU MCHAKATO UTAKAVYOKUWA



## IKIWA JAMII YENU INAO MWONGOZO TAYARI WA KUIFIKIA HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

Mnaweza kukabidhi nyaraka hiyo kwa wawekezaji na maofisa wa serikali na kuwaomba wafuate utaratibumliouchagua. Hata hivyo, sheria za majadiliano aumashauriano za nchi mwenu zinaweza zikaruhusu kampuni kuendelea na majukumu bila ya kuangalia mwongozo wenu kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Hii inafanya kusiwe na uzito katika mazungumzo yenu na mwekezaji au serikali kwa sababu hawawezi kutii mwongozo wenu kikamilifu. Kwa vyovyote, kuna uwezekano wa kukabiliwa na msukumo fulani - na hivyo kulazimika kuwa na majadiliano kuhusu mchakato wenyewe. Mnaweza kuendelea kusisitiza kuhusu haja ya kuwa na mchakato wa mazungumzo au kuachilia baadhi ya masuala endapo tu wataheshimu haki yenu ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

## IKIWA HAMNA MWONGOZO ULIOANDALIWA WA KUHUSU HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

Kuweni tayari kueleza namna ambavyo mndependa mchakato uwe. Tazama sehemu ya 2 kwa maelezo zaidi ya kina kuhusu mnachoweza kuomba.

## KAMA MWEKEZAJI NA/AU SERIKALI WANAGOMA KUFUATA MWONGOZO WENU WA HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

Ikitokea mwekezaji na/au serikali wanakataa kufuata mwongozo wenu, kukataa utaratibu uliowekwa, au kutaka kudhibiti mchakato wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, kuna hatua mnazoweza kuchukua kuhakikisha kuwa mwekezaji na/au serikali watafuata taratibu na viwango vya kimataifa vya kusimamia Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Mnaweza:

•Kubainisha sheria za nchi zinazohusu majadiliano na Watu wa Asili kuhusiana na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali Kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi na kusisitiza kuwa sheria hizo lazima ziheshimiwe. Hakikisha kuwa wawekezaji na maofisa wa serikali wanazijua sheria hizo zinazohusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi na sisitiza kuwa mchakato kwa ajili ya haki hiyo lazima ufuatwe.

**Kwa miradi ya uwekezaji, bainisha viwango vinavyotakiwa kuzingatiwa vya sekta husika kuhusiana na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi na simamieni utekelezwaji wa viwango hivyo.**

Baadhi ya tasnia zina bodi au mamlaka za kuzisimamia na zimeweka utaratibu wa kuwa na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Kama mwekezaji anagoma kutii matakwa ya sekta husika kuhusu viwango hivi vya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, mnaweza kuwafungulia mashtaka kwenye mamlaka zinazosimamia sekta husika. (Kwa mfano, kama ni mradi wa kuzalisha mafuta ya mawese, mnaweza kumtaka mwekezaji kufuata taratibu zilizowekwa na Mamlaka inayosimamia mafuta ya mawese, na kufungua mashtaka kwa mamlaka hiyo ikiwa mwekezaji amekiuka taratibu).

- Kwa miradi ya miundombinu ya serikali, watambue wanaofadhili miradi hiyo na mjue viwango vyao kuhusu haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi na muitake serikali kuzingatia viwango hivyo.
  Mara nyingi miradi ya serikali ya ujenzi wa miundombinu hufadhiliwa yote au kwa sehemu na benki za kimataifa, na kila mmoja akitaka matakwa yake kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi yazingatiwe. Kwa mfano, ikiwa mradi utafadhiliwa benki kadhaa za kimataifa na serikali haizingatii matakwa ya taasisi hizo za fedha, basi mnaweza kufungua madai na kuwasilisha kwenye taasisi hizo za fedha.
- Ikiwa mradi unaotekelezwa hauna mfadhili wa kimataifa na ndani ya sekta husika hakuna mamlaka ya kuusimamia, basi bainisheni mtu anayehusika na mradi na kumshinikiza afuate mwongozo wenu Haki
- ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Jamii yenu inaweza kushirikiana na vyombo vya habari vya ndani na vya kimataifa na asasi za kiraia kwa ajili ya kuomba msaada wa kuweka shinikizo kwa wahusika uliowabainisha.

Kama taratibu husika haziheshimiwi, kuna hatua nyingine za kuchukuliwa kwa ajili ya kukabiiana na ukiukwaji huo (Tazama sehemu ya 4 kwa taarifa zaidi kuhusu na namna ya kufungua malalamiko).

# TUNZENI KWA WAKATI NYARAKA ZA MCHAKATO

Ikionekana ni salama kufanya hivyo, ni vema kuweka kumbukumbu kwa njia ya video au sauti zinazohusu mikutano yote, na ikiwekezana hata kupiga picha. Unaweza kupakua kumbukumbu hizo kwenye majukwaa ya mtandaoni. Mnaweza pia kuwaalika wanahabari kufuatilia mchakato huo endapo itakuwa salama kwao kufanya hivyo. Ni vema kutunza kumbukumbu vizuri kwa ajili ya ushahidi utakaowapa nguvu ya kuweka msimamo wenu, lakini fahamuni kuwa nyaraka hizi zinaweza kumfanya mwekezaji au maofisa wa serikali kuanza kampeni ya vitisho, vurugu, au kuwalazimisha. Hili likitokea, ni muhimu kutunza ushahidi wa vitisho vyovyote —ingawa hili linaweza kuwaweka wanajamii katika hatari kubwa zaidi.

Shirikiana na mawakili na wanasheria katika kutafuta njia za kulinda ushahidi na nyaraka zenu: kwani siku hizi kuna njia za kufuta taarifa kwenye simu haraka, pamoja na mtandaoni, hivyo ni vema mkatunza vizuri video na picha zenu mahali usalama zaidi.



Kijana kutoka Jamii ya Watu wa Asili akirekodi majadiliano ya kwenye kikao na mwekezaji.

# HAKIKISHENI MNAKUWA NA TAARIFA ZA KUTOSHA

Hakikisheni mnao ufahamu na kuelewa wa kutosha kuhusu athari zote mbaya zinazoweza kutokea na matokeo ya mradi unaopendekezwa. Si vizuri kutegemea taarifa kutoka kwa wawekezaji na maofisa wa serikali pekee. Waandaaji wa mradi hujaribu kutoa picha nzuri ya mradi uonekane ni wa kuvutia ili wapate ridhaa yenu. Taarifa kutoka kwa vyanzo vingine zitawapa uelewa mpana zaidi kuhusu mradi pamoja na hatari na faida zake.

Manufaa ya uwekezaji yanaweza kujumuisha uboreshaji wa miundombinu (barabara, usambazaji wa maji na umeme, minara ya simu, shule, hospitali), ajira kwa wanajamii, kodi ya kila mwaka inayolipwa kwa jamii yenu, kiunganishi kati ya huduma na masoko, na manufaa mengine mtakayojadiliana.

Hata hivyo, mara nyingi:

- Hewa, udongo, na maji huchafuliwa, na hivyo kuhatarisha maisha ya wanyama na mimea;
- Mnaweza kupoteza haki yenu ya kutumia misitu, kufika kwenye vyanzo vya maji, kukosa ardhi ya malisho, maeneo ya uvuvi, na njia nyingine za kujikimu kimaisha yako, na ustawi wenu;
- Mnaweza kushinikizwa au kulazimishwa kuihama ardhi yenu;
- Barabara zinaweza kuchafua mazingira au kuhatarisha maisha ya watoto kwa malori makubwa kukatiza barabara siku nzima;
- Umeme na maji vinaweza kufika eneo la wekezaji lakini wananchi wasipate;
- Ahadi ya ajira inaweza kutotimizwa, kampuni inaweza kuajiri vibarua wa hali ya chinni kutoka kwenye jamii, na kazi zenyewe zikawa za muda mfupi, au wafanyakazi wasilipwe kwa miezi kadhaa;
- Wafanyakazi wa kampuni wanaweza kusababisha vurugu, pombe, dawa za kulevya na ukahaba katika jamii yenu, kubaka wanawake na watoto, kuhamisha rasilimali za eneo lenu bila ya utaratibu, kudai ardhi kwa matumizi yao wenyewe, na kusababisha hatari za kiafya na kiusalama kwa jamii, na haya yakiwa ni miongoni mwa matokeo mabaya ya uwekezaji.

Ili kufanya uamuzi sahihi wa ama kuridhia au kutoridhia kuwa na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi, ni muhimu kupata picha kamili ya mradi na athari zake zinazoweza kujitokeza. Kuna vyanzo mbalimbali vya taarifa ambavyo mnaweza kuvipitia. Vyanzo hivyo ni pamoja na:

1. Tathmini kamili ya athari za kimazingira na kijamii;
2. Nyaraka zote za mradi (*Tazama ukurasa wa 34*);
3. Uzoefu na ushauri kutoka kwa jamii nyingine zenye aina kama hiyo ya mradi (uchimbaji madini, ukataji magogo, biashara ya kilimo, utalii, kuvuna umeme wa upepo, n.k.);
4. Uzoefu na ushauri kutoka kwa jamii nyingine zenye miradi mingine ya mwekezaji huyu katika mikoa au nchi nyingine; na
5. Mnyororo mzima wa kampuni zilizowekeza, wafadhili, taasisi na benki zinazohusika na mradi.

Jamii yenu inaweza kutembelea jamii nyingine ili kujionea namna wanavyoishi na mradi sawa na huo wa kwenu. Mnaweza pia kufuatilia kama kuna kesi zilizofunguliwa dhidi ya mwekezaji, na matokeo ya kesi hizo.



## NYARAKA ZIPI ZA KUOMBA ILI KUPATA UFAHAMU WA KUTOSHA:

Mnaweza kuomba serikalini na/au kwa mwekezaji aina zifuatazo za nyaraka na taarifa:

1. **Mpango wa biashara wa mwekezaji:** Mara nyingi wawekezaji wanatakiwa kuwasilisha mpango wao wa biashara kwa serikali kabla ya kuanza mradi. Mpango wa biashara utatoa taarifa namna mwekezaji anavyopanga kuendeleza ardhi, ikiwa ni pamoja na mpango wa kina wa kazi na ratiba ya kazi. Mpango wa biashara unaweza pia kuonesha faida inayotarajiwa kupatikana kila mwaka na kwa muda fulani.
2. **Upembuzi yakinifu:** Sheria za nchi mara nyingi huwataka wawekezaji kufanya "upembuzi yakinifu" kwa ajili kuchunguza kama mradi unaopendekezwa unawezekana kufanyika na kama una faida.
3. **Vibali, leseni, na mikataba kati ya mwekezaji na serikali:** Wawekezaji mara nyingi wanapaswa kupata vibali au leseni maalumu kutoka serikalini. Wakati mwingine, mwekezaji anatakiwa atiliane mkataba na serikali kabla ya kuanza utekelezaji. Vibali kama hivyo, leseni na mkataba humlazimu mwekezaji kufanya (au kutofanya) mambo fulani kwenye ardhi ya jamii au iliyo jirani na eneo la mradi. Ikiwa tayari kuna mkataba kati ya mwekezaji na serikali, hilo linaweza kupunguza au kuongeza nafasi ya majadiliano na mwekezaji.

>> **Wanajamii wasihadaike na maneno ya mwekezaji kuwa ana kibali cha serikali cha kuendesha mradi wake** na wanatakiwa kuomba kuoneshwa nakala za nyaraka muhimu kama vile leseni au vibali. Kama mwekezaji anagoma, jamii inatakiwa kuomba taarifa hizo kutoka kwenye ofisi husika za serikali.

4. **Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii na ripoti zozote zinazohusu mazingira:** Ripoti za mazingira mara nyingi hufanywa hatua za awali za maandalizi ya mradi kabla ya tathmini kamili ya Athari za Kimazingira na Kijamii kufanyika. Ripoti hiyo huwa ni tathmini fupi ya hatari za mazingira za mradi, pamoja na mapendekezo ya namna ya kuepuka au kupunguza athari mbaya zinazoweza kutokea.
5. **Historia na rekodi za utendaji wa mwekezaji au ufanisi wake kwenye miradi mingine:** Wanajamii wangependa kuomba taarifa zinazohusu miradi mingine ya mwekezaji, ikiwa ni pamoja na nyaraka zinazooneesha jinsi miradi hiyo ilivyotekelezwa kwa muda husika. Taarifa hiyo itasaidia kujua namna kampuni inavyofanya kazi, ikiwa ni pamoja na kujua kama inaheshimu haki za binadamu na kufuata sheria za mazingira.

**Ili muweze kuelewa kilichoandikwa kwenye hizo nyaraka, mnaweza:**

Kuomba nyaraka hizo zitafsiriwe kwa usahihi katika lugha ya jamii ya asili na mfasiri asiyependelea/ asiyeegemea upande wowote na tafsiri hizo zipatikane kwa kuchapishwa au kusimuliwa kwa mdomo (kwa mfano, video au rekodi ya sauti ambayo wanajamii wanaweza kutazama au kusikiliza mara kwa mara);

Mnapewa muda wa kutosha na mnaouhitaji kwa ajili ya kupitia nyaraka hizo na kuzielewa;

Mnaachiwa nakala za nyaraka hizo. Kama hilo haliwezekani, basi pigeni picha za kila ukurasa wa nyaraka hizo kwa kutumia simu janja na kisha mtachapa kila ukurasa kwa ajili ya mapitio ya baadaye; Mnayo nafasi ya kuwauliza waendeshaji wa mradi maswali kuhusu nyaraka hizo;

na Wataalamu wa kiufundi na kisheria wanaowasaidia kazi washiriki kila mikutano yote ili taarifa fulani ikitolewa waweze kuuliza maswali na kudai maelezo ya ziada kwa niaba yenu. **Iwapo serikali au mwekezaji wanagoma kabisa kuwapa baadhi ya nyaraka hizo,** shirikianeni na wanasheria wenu, wasaidizi wa kisheria, au mawakili wenu ili kujua kama nchi au eneo lako liko ndani imepitisha Sheria ya Uhuru wa Habari ambayo inaruhusu wananchi kuomba taarifa serikalini.

# MJADILI MAMBO MUHIMU YA KUREKEBISHA KWENYE MRADI UNAOPENDEKEZWA KUEPUSHA HATARI NA MADHARA

Baada tu ya kupokea na kuelewa taarifa zote zinazohusu mradi, mwekezaji, na sheria zinazolinda haki zenu, ni vyema kufanya kazi na wanasheria, wataalamu wa kiufundi na mawakili kwa ajili ya:

- Kuandaa orodha ya hatari zote zinazotarajiwa za mradi na madhara yanayoweza kutokea;
- Kuandaa orodha ya sehemu gani za mradi mngependa zibadilishwe ili kupunguza hatari hizo; na
- Kuandaa orodha ya mambo ambayo jamii yenu ingependa yabadilishwe katika mradi ili kupunguza hatari (Msingoje mwekezaji au serikali ipendekeze mabadiliko—bainisheni ya kwenu).

Itafaa kuwagawia mwekezaji na maofisa wa serikali hiyo orodha mapema ili wajiandae vizuri kwa ajili ya majadiliano ya kina kuhusu hatari/madhara.

Kisha, wakati wa kukutana na waendeshaji wa mradi, jadilini kila hatari na madhara yanayoweza kutokea, ulizeni maswali yote, na muwabane watoe majibu sahihi na ya kueleweka. Jadilini jinsi mnavyoweza kurekebisha baadhi ya vipengele vya mradi ili kupunguza hatari. Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii itakuwa imetoa mapendekezo kuhusu hili, hivyo mnaweza kutumia tathmini hiyo kama msingi wa kuanzisha mabadiliko hayo kwa ajili ya kupunguza madhara ambayo ripoti inapendekeza, pamoja na mabadiliko mengine yoyote mnayoona ni muhimu kuwaepusha na madhara. Endeleeni kujadiliana hadi mjiridhishe kuwa mradi hautaharibu mazingira yenu, mfumo wa kiikolojia, vyanzo vya maji, udongo na hewa, afya, maeneo ya ibada za kimila, utamaduni, na ustawi wa jamii yenu. Mnaweza pia kujadiliana kuhusu mabadiliko kwenye mradi yatakayowanufaisha zaidi, kwa mfano, kutengeneza au kuanzisha miundombinu itakayoboresha maisha yenu.

**Uamuzi wa kushiriki katika mazungumzo (na mwekezaji) haimaanishi kwamba jamii yenu iko tayari kuingia katika makubaliano au kuridhia. Mazungumzo ni mchakato, na matokeo ya mwisho yatategemea kama wahusika watafikia makubaliano ya kuridhisha pande zote mbili.**



Baada ya kutumia haki yao ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiari kabla ya Kufanya Maamuzi, wanajamii wanapitia mpango wa biashara wa mwekezaji na kujadili iwapo wataridhia au hawataridhia mradi.

# MJADILI MASUALA YA FAIDA KWENU SERIKALI AU MWEKEZAJI LAZIMA WAYATOE MKIRIDHIA

Kumruhusu mwekezaji kutumia ardhi yenu kutaleta mabadiliko katika jamii yenu ambayo haitawezekana kuyarekebisha kwa pesa, kwa miundombinu, na kwa faida nyingine. Hata hivyo, endapo mtaamua kupatana kuhusu manufaa ambayo serikali au mwekezaji lazima wawape baada ya ninyi kuridhia ardhi na rasilimali zenu zitumike, lazima muweke wazi kuhusu mnachotaka mpewe, na kwamba lazima muweke bayana kwenye maelezo yenu. Kwa mfano, mkiomba kujengewa kituo cha kutolea huduma za afya, lazima mueleze kuwa siyo tu kuwa na kituo bali pia madaktari, manesi, vitanda, mashine, na dawa zinazohitajika ili huduma za afya zitolewe siku zote na zigharamiwe na mradi. Mara nyingi, serikali itatoa huduma za elimu na afya; jamii yenu inaweza kujadiliana na maofisa wa serikali na mwekezaji kuhusu manufaa hayo.

Ili kuelewa thamani ya faida mnazoweza kuomba, mnaweza:

- Mjue faida ya kila mwaka ambayo wawekezaji wanatarajia kupata;
- Chunguzeni thamani ya ardhi kwenye maeneo ya mijini na vijijini kwenye nchi yenu, na nchi zinazowazunguka, ili mjue thamani halisi ya ardhi ilivyo kwenye soko; na
- Fanyeni zoezi la Uthamini katika Kiambatisho C ili kuelewa thamani ya soko ya rasilimali mtakazopoteza mkiamua kuampa mwekezaji au serikali ardhi waliyoomba.

Faida unazoweza kuomba ni pamoja na:

**Malipo ya kukodisha na kugawana faida, kama vile:**

- Kurudia malipo kama vile kodi ya kupangisha ya kila mwaka pamoja na marekebisho yake kuendana na kuporomoka kwa thamani ya pesa, gharama za bidhaa za kimsingi kama vile nafaka. Kwa mfano, dola 1 katika uchumi wa leo inaweza kupoteza nusu ya thamani yake katika miaka 20 ijayo; hivyo kuweka malipo kwa gharama ya bidhaa kwa kuhakikisha kwamba kadiri sarafu inavyopoteza thamani yake, malipo yenu ya ukodishaji yanabaki na thamani mliyopatana hapo awali;
- Sehemu isiyobadilika ya faida ya kila mwaka ya kampuni; na
- Mgawo wa hisa za kampuni, na aina nyinginezo za malipo ya kifedha.

## KUWA MAKINI!

Mkishajadiliana kuhusu mrabaha wa kila mwaka, lazima mtengeneze mifumo ya kuhakikisha pesa hizo zinatumika kama ilivyotarajiwa, na mnaweka njia za kudhibiti matumizi yake na kuhakikisha kuna uwazi, usawa na haki katika matumizi yake.

**Uendelezaji wa miundombinu au huduma za kijamii (pamoja na yale yaliyokuwa yamepangwa kwa ajili ya uendeshaji wa uwekezaji wenyewe), kama vile:**

- Kituo cha kutolea huduma za afya pamoja na wafanyakazi na vifaa vyote muhimu (madaktari, wauguzi, mashine, dawa, vitanda, n.k.);
- Shule na wafanyakazi na vifaa vyote muhimu (walimu, madawati, ubao, vitabu, karatasi, n.k.);
- Umeme unaotokana na nishati mbadala (zisizo za mafuta) kama vile umeme wa maji, upepo, au jua kwenye majengo na nyumba zote;
- Maji, kama vile visima vya ziada na/au majia ya bomba kwenye nyumba na majengo;
- Miundombinu ya mawasiliano; na
- Kuboresha miundombinu utoaji wa huduma kwa jamii, kama vile barabara mpya/bora na madaraja.

> Mkiomba kujengewa miundombinu mipya, hakikisha maombi yanakuwa na maelezo ya kina kama vile: ni nani atakayeijenga, tarehe ya ukomo wa kazi, malighafi zitakazotumika, mahali itakakojengwa, matengenezo ya mara kwa mara yanayohitajika ili kuifanya ifanye kazi kwa usalama na kikamilifu, na ni nani atakayewalipa wafanyakazi wanaohitajika. Pia hakikisheni mnajumuisha adhabu kwenye makubaliano yenu endapo mwekezaji hatakamilisha mradi wa miundombinu kulingana na ratiba iliyokubaliwa.

**Kazi na mafunzo ya kiufundi, pamoja na:**

- Kuwepo na idadi maalum ya nafasi za kazi za muda mrefu na muda mfupi, na idadi fulani ya kazi za ujuzi (kama vile nafasi za utawala au kazi za ofisi) kwa wanajamii wa Asili;
- Nafasi za kazi zitolewe kwa makundi yote ya watu wa asili, wakiwemo wanawake na vijana;
- Asilimia maalumu ya wafanyakazi wa kampuni ijumuishe wanajamii (Kukiwa na wafanyakazi wengi kutoka na jamii za nje kunaweza kuwa na athari mbaya kwa jamii yenu);
- Mafunzo ya kiufundi yatolewe ili wanajamii waweze kujaza nafasi zilizopo, zikiwemo za utawala na ujuzi mbalimbali;
- Kila mwaka kuwepo na idadi fulani ya ufadhili wa masomo kwa ajili ya vijana wa jamii yenu kwenda kusoma shule za sekondari na chuo kikuu, endapo jamii yenu itaona inafaa; na
- Mikataba ya upendeleo kwa wanajamii (kwa mfano, kuwapikia wafanyakazi chakula cha mchana au kuchangia vitendeakazi kwa ajili ya uendeshaji wa mradi, miongoni mwa manufaa mengine).

Kuweni bayana katika madai yenu: Wawekezaji mara nyingi huahidi kutengeneza ajira nyingi kwa wanajamii, lakini kiuhalisia huajiri watu wachache sana kutoka kwenye jamii, au huwaajiri wana jamii wengi na kutokuwalipa vizuri. Wanajamii wanapoomba mwekezaji atengeneze ajira inabidi pia waombe: mishahara mahususi kwa kila aina ya kazi, marupurupu mbalimbali yanayotokana na ajira, na nini kifanyike ikiwa mishahara haitalipwa kwa wakati. Mnaweza pia kujadili kuhusu viwango vya mazingira ya kufanyia kazi, ikiwemo saa za kazi, matibabu, na adhabu kwa kunyanyasa mfanyakazi au mazingira duni ya kazi

# F A N Y E N I M A A M U Z I

Baada ya jamii yenu kuwa na taarifa zote muhimu, imezielewa hatari zote, na kushiriki kikamilifu katika mchakato mashauriano na mapatano na kampuni husika, sasa mtakuwa tayari kujadili mradi huo ninyi wenyewe na kuamua kuridhia au kutoridhia haki yenu ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi.

**Fanyeni maamuzi kulingana na taratibu zenu za kijadi.**

Jamii yenu inayo haki ya kufanya maamuzi kwa mujibu wa taratibu zenu za jadi za kufanya maamuzi. Katika kila nyanja, jamii yenu inayo haki ya kujiamulia mambo, ikiwepo pia haki ya namna ya kufanya maamuzi. Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi ni haki ya pamoja: kutokana na taratibu zenu za kijadi, ni jambo muhimu kuhusisha wanajamii wote kwenye maamuzi. Kama ilivyoelezwa hapo juu, michakato ya uwazi na ya pamoja ya kufanya maamuzi inayohakikisha ushiriki sawa wa wanajamii wote inaweza kuwasaidia kufikia maamuzi bora kwa ajili yenu.

**Kama mmeridhia au hamjaridhia, basi wekeni kwenye maandishi uamuzi wenu.** Mara tu baada ya jamii yenu kufanya maamuzi, wekeni katika maandishi huo uamuzi wenu na pigeni picha na video, kadiri inavyofaa katika utamaduni wenu. Nyaraka hiyo ya maandishi lazima ieleze bayana kama mmeridhia au hamjaridhia na hakikisheni uamuzi huo ni dhahiri na unatekelezeka. Ikiwa mmeamua kuuridhia mradi, basi mnatakiwa kuambatanisha hati hiyo ya idhini (kama kiambatisho) yenye masharti ya ridhaa yenu, na kila kitu ambacho mmekubaliana na mwekezaji na/ au serikali. Huo unaweza kuwa msingi wa mkataba wa kimaandishi. Mnaweza pia kujumuisha mashaka yoyote kuhusu malalamiko au mzozo unaoweza kutokea huko mbeleni.

Hati hii inaweza kutolewa kwa mwekezaji, serikalini, na wote wanaosimamia mradi na wafadhili. Inaweza kuwa jambo la maana endapo nyaraka hizo zitatolewa pia jamii jirani pamoja na vyombo vya habari ndani ya nchi na vya kimataifa, lakini pia mnaweza kuwapa washirika wengine mnaoamini wanastahili kupewa nakala.

**Endapo mtakuwa mmeamua kuuridhia mradi, hakikisheni kuwa makubaliano yenu yanaandikwa kisheria kwa njia ya mkataba** na mwekezaji, mwendeshaji wa mradi na/au serikali ambao utakuwa umegusia kila kipengele cha makubaliano. Tazama Sehemu ya 4 kwa maelezo zaidi kuhusu kuandikiana mkataba rasmi.

## HAKUNA RIDHAA HALALI ENDAPO WANAJAMII WATAHISI KUSHINIKIZWA

Ili mashauriano na ridhaa viwe "huru," Watu wa Asili kamwe wasilazimishwe wakati wa kupatana kushauriana. Hii ni pamoja na kuonesha vitisho vya kutumia nguvu au kulipiza kisasi, pamoja na hongo na aina nyinginezo za ufisadi. Ikiwa jamii yenu inahisi kushinikizwa kukubali, wekeni kumbukumbu ya mnachokutana nacho (ikiwa ni salama kufanya hivyo). Mnaweza kupinga mchakato huo mahakamani na kuweza kubatilisha ridhaa yenu.

## BADO UNAWEZA KUSEMA HAPANA HATA BAADA YA KUKAMILISHA MAPATANO

Ni haki yenu kujadili kikamilifu kila kipengele cha mradi, ikiwa ni pamoja na mabadiliko gani yanapaswa kufanywa kwa mradi ili kupunguza hatari na ni faida gani zitalipwa kwa jamii yenu, na kisha, mwishoni, mtaamua kutoridhia mradi.

## MNAWEZA KUGOMEA BAADHI YA VIPENGELE VYA MRADI NA KURIDHIA VIPENGELE VINGINE

Kulingana na mradi, jamii yenu inaweza kukubali baadhi ya vipengele na kukataa vingine. Kwa mfano, mnaweza kukubali kiwanda cha uchakataji lakini mkakataa kuridhia shughuli za uchimbaji madini au biashara ya kilimo zinazozalisha malighafi za mradi, au kinyume chake.



Wanajamii wakigomea haki ya kujulishwa, kuelewa na kuamua kwa hiyari kabla ya kufanywa kwa uamuzi.

## HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI NA UKOMO WA SHERIA ZA NCHI

Wakati baadhi ya nchi zimepitisha sheria zinazohusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi au mchakato wa majadiliano na Watu wa Asili, hakuna nchi inayotetea haki hizo za Watu wa Asili kwa viwango vya chini vilivyowekwa na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu wa Asili.

Iwapo sheria na kanuni za nchi yenu zinatambua ardhi au eneo la Watu wa Asili na kutambua Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kama sharti la kuridhia mradi, basi kupinga kwenu mradi kunaweza kufanyika kikamilifu ili usifanyike ndani ya eneo lenu. Katika nchi nyingine, mchakato wa mashauriano ndio pekee unaohitajika kisheria, bila kujali jamii yenu itaamua nini. Baadhi ya nchi zinaelekza kwanza kuwepo kwa ridhaa ya jamii ya Watu wa Asili kuhusu Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi kwa miradi ya biashara ya kilimo, ukataji magogo na nishati mbadala ili kuendelea, lakini si kwa miradi ya uchimbaji madini (katika nchi nyingi, serikali ndiyo inayomiliki mali zote zilizo chini ya ardhi). **Mkiamua kutoridhia, tafuteni ushauri wa kisheria ili kuelewa nguvu ya kusheria ya uamuzi wenu wa kutoridhia mradi.**



**Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi ni haki ya pamoja: kwa kuendana na michakato yenu ya jadi, ni vema kushirikisha wanajamii wote kwenye maamuzi. Uwazi, michakato shirikishi ya kufanya maamuzi vinaweza kuisaidia jamii yenu kufanya maamuzi bora kwa ajili ya jamii yenu.**

# BAADA YA MAAMUZI KUHUSU HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI: HATUA ZINAZOFUATA

# 04




Jamii ya Watu wa Asili ikipinga mahakamani ulaghai katika mchakato wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.

Mkishaamua kama jamii kuridhia au kutoridhia mradi, kuna aina mbalimbali za hatua za ufuatiliaji ambazo mnaweza kuizichukua au kutakiwa kuzichukua. Endapo mlikataa kuridhia, mtatakiwa kuchukua hatua za kisheria kwa kutangaza hadharani au kuchukua hatua za kisiasa ili uamuzi wenu uheshimiwe. Iwapo mmeridhia, basi mhakikishe kuwa masharti ya mkataba wenu yameandikwa kisheria na kuweka wazi taratibu za ufuatiliaji, kushughulikia malalamiko, na mikakati ya utatuzi wa migogoro. Masuala haya yamefafanuliwa kwa ufupi kwenye kurasa zinazofuata.

**BAADHI YA MIKAKATI INAWEZA KUWA HATARISHI KWA WANAJAMII. TAFUTENI USHAURI WA KISHERIA**

Tafuteni ushauri wa kisheria kwa ajili ya kupata uelewa wa uhakika kuhusu madhara yanayoweza kutokea ya kisheria, kisiasa, kijamii, kiuchumi na kimwili ya kila mkakati unaopendekezwa. Kwa mfano, kukataa kuridhia na kuendelea kuupinga mradi kunaweza kuhatarisha usalama wa viongozi wa jamii yenu na wanajamii, na kunaweza kusababisha kuwekwa kizuizini au kubambikiziwa kesi za jinai.

# MKIKATAA: HAKIKISHENI KUKATAA KWENU KUMEKUBALIKA

Iwapo jamii yenu haitaridhia mradi, tafuteni ushauri wa kisheria kuhusu haki zenu kupitia sheria za ndani ya nchi. Mwanasheria anaweza kuishauri jamii yenu kuhusu mikakati ya kisheria ambayo mnaweza kuitumia kusimamia haki yenu ya kuukataa mradi.

Iwapo jamii yenu haina haki kisheria kuukataa mradi - kwa mfano, kuhusu mradi wa uchimbaji madini katika nchi ambayo serikali inashikilia haki zote za maliasili zilizo chini ya ardhi na haijatoa tamko la kupitisha sheria ya kutambua Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi - bado mnaweza kutafuta au kutumia mikakati mingine ya kupinga mradi usiendelee. Jamii yenu inaweza kutumia mikakati na michakato ifuatayo:

## 1.KUFUNGUA KESI MAHAKAMANI

Jamii yenu inaweza kufungua kesi mahakamani ili: kutetea au kuomba kutambuliwa zaidi kwa haki yenu ya kujiamulia mambo kama jamii, kutambua rasmi haki yenu ya kutoridhia mradi, au kupinga uhalali wa maamuzi ya serikali ya kutoa kibali kwa kampuni kuanzisha mradi. Mnaweza kujitetea kwamba mradi huo unatishia maisha yenu kama Watu wa Asili, zikiwa ni miongoni mwa hoja nyingi zinazoweza kutumika kujenga hoja za kisheria.

## 2. MICHAKATO YA TATHMINI ZA KUJIRIDHISHA NDANI YA SHIRIKA

Fanyeni kazi na mwanasheria au Shirika lisilo la Kiserikali ili muweze kujifunza kuhusu taratibu za kujiridhisha ambazo mwekezaji anapaswa kufuata wakati wote wa maisha ya mradi. Mnaweza kuibua malalamiko au kupinga matokeo ya tathmini hizo.

## 3.MIFUMO ISIYO YA KIMAHAKAMA YA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

Mnaweza kutumia viwango vya kimataifa vya sekta au itifaki za benki za maendeleo ili kusimamisha mradi uliopangwa wa mwekezaji. Ombeni ushauri wa kisheria kuhusu:

- Endapo kuna viwango vyovyote vya usimamizi ndani ya sekta au benki ya maendeleo vinavyosimamia mradi;
- Kama kuna utaratibu wa malalamiko unaohusiana na viwango hivyo; na
- Ni suluhu zipi au taratibu zipi zinazoweza kutumika endapo mtafungua jalada la malalamiko kwa ajili kuomba kuusimamisha mradi/kulinda jamii yenu dhidi ya madhara.

Kunaweza kuwa na malalamiko zaidi moja ambayo mnaweza kuyafungulia majalada ya malalamiko.

## 4. UCHECHEMUZI

Uchechemuzi mi kampeni ya utetezi inaweza kusaidia kuongeza ufahamu wa jamii yenu kuhusu kutoridhia mradi, pamoja na nguvu yoyote, vitisho, vurugu, au kushurutishwa ambako jamii yenu imekumbana navyo katika kipindi cha kujadiliana kuhusu haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Ili kampeni ya uchechemuzi ya utetezi iweze kuwa na mafanikio inanidi kumshinikiza mwekezaji na/au serikali kusitisha au kubadilisha mradi na kufanyia kazi matatizo yenu kikamilifu. Ushawishi unahusisha kuwafikia maofisa wa serikali wanaoaminika au maafisa wa kampuni ambao wanaweza kutetea madai yenu.

Wakati wa kujiandaa kwa ajili ya kampeni ya utetezi, ni muhimu sana kuwa na picha kamili ya mnyororo wa uwekezaji wa mradi (Tazama Sehemu ya 2 ukurasa wa 27 kwa orodha kamili ya wanaoweza kuwa katika mnyororo wa uwekezaji.) Jamii yenu inaweza pia kuwasiliana na makampuni ya bima yanayosimamia uendeshaji wa kampuni. Huu ni mkakati madhubuti sana: ikiwa unaweza kuthibitisha kuwa mwekezaji amekiuka sera za bima, ushahidi unaweza kumfanya mtoa bima kujiondoa au kurekebisha masharti. **Bila bima ya hatari, miradi haiwezi kuendelea na uendeshaji.**

Jamii yenu inaweza kushirikiana na waaandishi wa habari wa kimataifa na Mashirika yasiyo ya Serikali ya kimataifa yanayofanya kazi zinazoendana na mtazamo wenu. Vyombo vya habari vya kimataifa vina nafasi kubwa ya kutangaza hali manayopitia, kwani waandishi wa kitaifa wanaweza kuwa hatarini au kuadhibiwa kwa kufanya hivyo. Fanyeni kazi na wanaharakati wakongwe ili wawape mbinu zaitakazowaletea mafanikio zaidi. Mitandao ya kijamii ina nguvu sana; kampeni ya mitandao ya kijamii itafika kwa watu wengi sana na watajua kuhusu madhara na ukiukaji wa haki unaofanywa na kampuni, na baadaye ikafanya mabadiliko ya namna inavyofanya kazi na kurekebisha kasoro zake ili kulinda heshima kwa taasisi za fedha.

### 5. KUKABILIANA BILA YA KUTUMIA VURUGU

Hatua za kukabiliana bila ya vurugu ni pamoja na maandamano na aina nyingine za hatua za amani zinazofanywa na wanajamii. Jitihada kama hizi zinaweza kusaidia kutangaza malalamiko yenu na, katika mazingira fulani, kuchelewesha au kusimamisha kabisa shughuli za kampuni. Hata hivyo, hatua hizi zinaweza kuchukuliwa kuwa haramu katika nchi yenu, na hivyo kuwaweka wanajamii katika hatari ya kufungwa jela au kufunguliwa mashtaka ya jinai na kunyanyaswa au kufanyiwa ukatili na vikosi vya usalama.

# KAMA MMERIDHIA: HAKIKISHENI MNALINDA HAKI ZENU

## MAJADILIANO UHUSU MKATABA

Masharti yanayohusu haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi yanayotolewa na Watuwa Asili yanachukuliwa kama “makubaliano,” l akini huu ni udhaifu wa sheria. “Makubaliano” hupunguza nguvu ya kisheria ya kutekeleza mlichokubaliana na kukifanya kisiwe na nguvu ya utekelezaji. Hata kama jamii yenu ilikuja na masharti mazuri wakati wa majadiliano kuhusiana na mradi, ikiwa masharti hayo hayatawekwa kwenye mkataba unaolindwa na sheria za kitaifa na kimataifa, mnaweza kuwa changamoto ya kuyatekeleza.

Iwapo jamii yenu itaamua kuuridhia mradi, ni vema kuweka kwenye kumbukumbu makubaliano na mazungumzo yenu yaliyowezesha kufikia uamuzi wa kuridhia na kuweka kwenye mkataba ambao umeandaliwa na kutiwa saini na wahusika wote. Mwekezaji na maofisa wa serikali wanaweza kukwepa kuandika mkataba kwa sababu ya kuweza kutumika kama ushahidi mahakamani, wakisisitiza kuwa mashauriano mliyofanya yanatosha kuwa “makubaliano.” Sisitizeni kuhusu kuwa na mkataba uliosainiwa na na fuatilieni kuhakikisha mkataba unasainiwa.

Mara nyingi mikataba huandikwa kwa lugha ngumu ya kisheria ambalafuteni msaada na ushauri wa wawasaidizi sheria, yo ni ngumu sana kuelewa. Maweza kudai mkataba uandikwe kwa lugha nyepesi, rahisi ambayo inayoweza kueleweka kwa urahisi na wanajamii wa Asili (ambao lazima watii mkataba) na mafisa wa serikali ya mtaa (ambao wanaweza kuitwa kutekeleza masharti ya mkataba). Mkataba ulioandikwa kwa lugha rahisi una nguvu sawa ya kutekelezeka. Mnaweza pia kudai mkataba utafsiriwe kwa lugha yenu.wanasheria, wataalamu, na mawakili wengine unapofanya kazi na wawekezaji na/ au maofisa wa serikali kuandaa na kukamilisha mkataba.

Mada inayohusu majadiliano ya mkataba ni pana na ya kina. Fanyeni kazi pamoja na wataalamu wenu wa sheria wakati wa kuandaa mkataba. Hata hivyo, kuna masuala kadhaa mnapaswa kuwa waangalifu sana:

- Thibitisha kwamba mkataba una kifungu cha muda mfupi wa uhalali, na kwamba mkataba huo utajadiliwa upya kila baada ya miaka mitano, kwa mfano. Duniani kote, kuna mifano mingi ya mikataba ya uwekezaji ambayo ina muda wa miaka 50 au 100, ambayo ina maana kwamba hakuna uwezekano wa kujadili upya masharti ya mkataba kwa vizazi vingi. Ingawa mwekezaji anaweza kutamani kuwa na mkataba wa muda mrefu, mna haki ya kukubaliana kuwa mkataba utadumu kwa miaka michache tu, na kutakuwa na nafasi ya kuendelea baada ya kufanya tathmini na kuwa na awamu nyingine ya mazungumzo kuhusu masharti.
- **Mjadili kwa umakini kuhusiana na mkakati wa kuufuata wakati kampuni inafunga shughuli zake baada ya mradi kwisha.** Mtahitaji kuona mkataba unaeleza bayana kuwa:
- Ardhi itarejea kuwa chini ya usimamizi wa jamii mradi utakapokwisha.
- Kampuni au serikali ianishe mipango yake ya kuhakikisha mradi unapoisha, jamii yenu inakuwa na maji safi, ardhi inarejeshwa kwenye ubora, bioanuwai inayostawim (kulingana na matakwa yenu). Mkataba unaweza kuelekeza kuwa kampuni isafishe, kurejesha, na kutengeneza upya ardhi ili wanajamii waweze kuitumia kama ilivyokuwa kabla ya mradi kuanza.
- Hakikishrni kuwa mkataba unaeleza wazi kwamba jamii yenu inayo haki ya kujiondoa katika uamuzi wa awali wa kuridhia mradi endapo shughuli zilizopendekezwa za mradi zitabadilika, ikiwa serikali au mwekezaji wamekiuka vipengele vya mkataba, au kukitokea taarifa mpya ambazo hamkutolea maamuzi hapo awali.
- Mnaweza kuongeza katika mkataba kipengele cha kuwa ni lazima mjulishwe iwapo kutakuwa na utafiti mpya au kutakuwa na data mpya zikionesha kuwa shughuli za mradi zitakuwa na madhara au hatari kwenu.



# NINI KIINGIZWE KWENYE MKATABA?

Mikataba inaweza kuwa na vipengele vingi tofauti - ikiwa ni pamoja na masuala mliyokubaliana na serikali/wawekezaji lakini mambo ya msingi ambayo lazima yajumuishwe katika mkataba kati yenu na mwekezaji ni:

1. Wahusika kwenye mkataba
2. Nia yako ya kufungwa kisheria na vifungu vya mkataba
3. Maelezo kamili ya mradi
4. Muda wa mkataba na uwezekano wa kufanyiwa mapitio
5. Maelezo na mipaka ya eneo lililotolewa kwa ajili ya mradi
6. Haki za kila upande ndani na karibu na eneo lililotengwa kwa ajili ya mradi
7. Maelezo kamili ya miundombinu ya mradi
8. Mambo ambayo kampuni itatoa kwa jamii yenu kwa kuridhia ardhi na rasilimali zenu
9. Mchakato wa tathmini yoyote ya athari na fidia kwa uharibifu
10. Makubaliano kuhusu kulinda mazingira dhidi ya uharibifu na madhara kwa kiafya ya binadamu
11. Ulinzi uliokubaliwa dhidi ya uharibifu wa kijamii na kitamaduni, pamoja na sheria za tabia ya wafanyikazi wa kampuni
12. Mchakato wa kutoa taarifa- ikiwa ni pamoja na taarifa za kampuni- wakati wa uwekezaji
13. Mgawanyo wa haki
14. Mapitio, mazungumzo mapya, na marekebisho ya mkataba
15. Utaratibu uliokubalika wa ufuatiliaji
16. Michakato ya kusuluhisha migogoro na kufikisha malalamiko
17. Ni sheria zipi zitasimamia mkataba
18. Namna ya kutoa notisi
19. Fidia: Kitu gani kitatokea ikiwa kampuni imekiuka mkataba?
20. Sababu na taratibu za kusitisha mkataba
21. Matukio yasiyotarajiwa (force majeure)
22. Nini kitatokea kwa ardhi na uboreshaji baada ya mkataba kumalizika (ugawaji wa mali)
23. Usiri, kifungu kizima cha makubaliano, na saini.



## MICHAKATO YA UFUATILIAJI NA UZINGATIAJI WA SHERIA

Ni muhimu sana kwa jamii yenu ianzishe mpango wa kina wa ufuatiliaji na uzingatiaji wa makubaliano nkama sehemu ya haki yenu Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Hii inajumuisha sehemu tatu:

1. **Mawasiliano ya wazi na mazungumzo ya mara kwa mara.** Kama Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi ni mchakato endelevu, mnahitaji kufahamishwa mara kwa mara kuhusu maendeleo ya mradi na kupewa fursa za kuuliza maswali, kuibua mashaka, na kukagua shughuli za mradi. Mnaweza kurekebisha vipengele vya mwongozo wenu kuhusu haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi kuwa mpango wa kina wa mawasiliano utakaojumuishwa kwenye mkataba wenu. Itafaa endapo mtaweka wazi ratiba ya mikutano ya kawaida, na matukio muhimu, matatizo, au masuala yatakayosabisha mkutano maalumu.

2. **Ni haki yenu kufuatilia shughuli zote za mradi wakati wote wa uwepo wake, ikiwa ni pamoja na:**
   - Kujua kama kampuni inatekeleza mradi wake kwa mujibu wa masharti yaliyokubaliwa wakati wa majadiliano kuhusu HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI;
   - Athari za mradi kwa ardhi yenu, udongo, hewa, maji, wanyama, mimea na mifumo ya ikolojia;
   - Athari za mradi kwenye utamaduni wenu, mfumo wa kijamii, usalama, afya na haki za binadamu;
   - Tabia ya wafanyakazi wa kampuni kwenye jamii yenu;
   - Iwapo mwekezaji analipa fidia iliyokubaliwa na kuweka miundombinu yote iliyokubaliwa kwa ubora na kwa muda uliokubaliwa;
   - Iwapo mwekezaji anapanua shughuli nje ya mipaka iliyokubaliwa ya shughuli; na
   - Athari zozote chanya au hasi zisizotarajiwa.



Wanajamii wakifuatilia kama mwekezaji anazingatia vifungu vya mkataba/uwekezaji.

Kwa kukubaliana kuhusu utaratibu wa kufanya ufuatiliaji, ninyi pamoja na waendelezaji wa mradi mnaweza kushughulikia kwa haraka masuala yoyote yanayojitokeza.

Mpango wa ufuatiliaji unaweza kujumuisha:

- Nani atakuwa anafanya ufuatiliaji (ikiwezekana: wanajamii waliopata mafunzo na wanaolipwa, wakisaidiwa na wataalamu wa kiufundi wasiopendelea upande wowote);
- Ufuatiliaji utafanyika mara ngapi (unaweza kufanyika kila siku, kila wiki, au kila mwezi kutegemeana na hali ya uchafuzi wa mazingira na mambo mengine hatarishi kwa jamii yenu);
- Mtafuatilia vitu gani (udongo, hewa, bioanuwai ya mimea, ubora wa maji, aina za wanyama, pesa zinazolipwa kwenye akaunti ya benki ya jamii,maendeleo ya ujenzi wa miundombinu, n.k.);
- Jinsi matokeo ya ufuatiliaji wote yatawasilishwa kwa kampuni na wanajamii wote; na
- Mtakakohifadhi data zote za ufuatiliaji (zihifadhiwe sehemu ya usalama ili zisipotee, ikiwezekana zitolewe kwa umma); na masuala mengine yoyote muhimu kwa jamii yenu.

**3. Mwekezaji kutii sheria.** Hakikisheni kwamba mkataba unaeleza kwa uwazi kile ambacho lazima kifanyike ikiwa ufuatiliaji utafichua uharibifu wa mazingira, kuhatarisha afya, ukiukwaji wa haki za binadamu na athari zingine mbaya. Makubaliano hayo yanapaswa kubainisha kile ambacho mwekezaji na/au serikali watafanya katika ikitokea data zinaonyesha uchafuzi wa mazingira kinyume cha sheria, ukiukwaji wa mkataba na changamoto nyingine.



Wanajamii wakianzisha mchakato wa kuwasilisha malalamiko.

## RIDHAA INAYOBADILIKA KUENDANA NA MABADILIKO YANAYOTOKEA KWENYE MRADI

**Haki Ya Kujulishwa, Kuelewa Na Kukubali Kwa Hiyari Kabla Ya Kufanya Maamuzi siyo jambo la kutolewa mara moja, bali ni mchakato endelevu unaotakiwa kurudiwa kadiri mradi unavyoendelea.** Waendelezaji wa mradi na maofisa husika wa serikali wanapaswa kushauriana na jamii yenu na kupata haki yenu ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi ya kila hatua mpya ya mradi, na kabla ya mabadiliko makubwa kufanywa katika mradi. Ridhaa yenu mliyotoa ilikuwa kwa mradi wa awali: ikiwa mradi utabadilishwa kwa kiasi kikubwa, basi ridhaa ile haihusiani na mabadiliko hayo. Katika mkataba wenu, mnaweza kueleza bayana masharti yatakayojadiliwa wakati wa mchakato wa kukubaliana kuhusu ridhaa na makubaliano hayo lazima yajadiliwe upya. Masharti hayo yanaweza kujumuisha masuala ya:

- **Wamiliki wapya au wasimamizi wa mradi**. Umiliki wa miradi ya uwekezaji mara nyingi hubadilika. Wawekezaji mliojadiliana nao wanaweza kuuza biashara hiyo kwa kampuni nyingine. Wasimamizi wa kampuni mpya wanapaswa kutekeleza ahadi zilizotolewa na wamiliki na wasimamizi waliotangulia—lakini wanaweza kukwepa kufanya hivyo. Mnaweza kudai mkataba ueleze wazi kwamba ikiwa mradi utauzwa kwa kampuni mpya, basi mmiliki mpya anafungwa na mkataba uliopo wa mwekezaji wa awali na jamii yenu.
- **Mabadiliko makubwa ya uendeshaji**, kwa mfano, vifaa vipya, malighafi mpya, kemikali za usindikaji mpya, n.k.
- **Mabadiliko makubwa ya matumizi ya ardhi na rasilimali zenu** na mabadiliko yoyote makubwa ambayo mnawez kutarajia. Mkataba wenu unaweza kuweka msingi wa:



## TARATIBU ZA KUPOKEA MALALAMIKO NA UTATUZI WA MIGOGORO

**Ikiwa mwekezaji na/au serikali hawatatua changamoto, ukiukaji na/au vitendo vya ukatili, basi jamii yenu ina haki ya kuanzisha mchakato wa kuwasilisha malalamiko na/au kutatua mgogoro.** Hakikisheni kuwa mkataba unajumuisha taratibu za kina za kufikisha malalamiko na utatuzi wa migogoro.

Utaratibu wa kuwasilisha malalamiko (manung'uniko) ni mchakato ambao watu walioathiriwa wanaweza kuwasilisha malalamiko yao kuhusu mradi - kwa kampuni, serikali, wafadhili wa mradi, au mamlaka inayosimamia sekta husika - na kuomba tatizo litatuliwe. Ikiwa umeandaliwa vizuri, utaratibu wa kushughulikia malalamiko unaweza kuwa rahisi kwa viongozi na wanajamii za asili kuutumia, unaweza kusaidia kutatua matatizo kwa haraka zaidi kuliko kutumia njia ya kufungua madai mahakamani, na hauleti mapambano.

Utaratibu mzuri wa malalamiko hufaa zaidi kwani: unakuwepo kirahisi, unajitegemea na hauna kupendelea; ni wa haki na na usawa na matokeo yake ni mazuri; una uwazi, uwajibikaji, na wenye weledi; una ufanisi na madhubuti; unafaa kiutamaduni; na unahusisha washauri wa kitaalamu inapobidi.

Namna wanajamii wanaweza kuwasilisha malalamiko:

- nani wa kupokea malalamiko na ushahidi upi unaohitajika kuambatana na malalamiko;
- Utaratibu utakaowekwa wa kufikisha mkataba huo kwa jamii yenu, kwa lugha yenu, na kwa kuzingatia utamaduni wenu;
- Uchunguzi utakaofanywa na kampuni kuhusu malalamiko na kuwasaidia wanajamii kupata taarifa yoyote wanayohitaji ili kutoa ushahidi wa malalamiko yao;
- Namna ambavyo malalamiko yatafanyiwa maamuzi na kutekelezwa. Mnaweza kudai kuwepo na wawakilishi wenu kwenye jopo litakaloshughulikia malalamiko hayo;
- Kuwalinda wanajamii wanaoleta malalamiko dhidi ya vitendo vya kulipiza kisasi;
- Hata kama kutakuwepo na utaratibu wa kupokea malalamiko, bado jamii yenu itakuwa na haki ya kufungua madai mahakamani; na
- Masuala mengine yoyote ambayo jamii yenu inafikiri ni muhimu.

**Taratibu za utatuzi wa migogoro zinaweza kutumika pale ambapo kuna kutokuelewana kati yenu na waendelezaji wa mradi.** Katika mkataba mnaweza kuweka kifungu cha utaratibu wa utatuzi wa migogoro:

- Unaoendana na taratibu zenu za kijadi za utatuzi wa migogoro;
- Ufanyike katika jamii yenu, kwa lugha yenu, na kulingana na muda na kasi mnayopendelea; na
- Wasuluhishi wa migogoro hiyo ni wazee na viongozi wanaoheshimika, au ninyi na kampuni mnawateua wasuluhishi.

Mnaweza pia kuamua kuwa mchakato wowote wa utatuzi wa migogoro lazima uanze na upatanishi au usuluhishi ndani ya jamii yenu, na kisha mnaweza kukata rufaa hadi kufikisha ma-hakamani, hadi ngazi ya mahakama kuu na mahakama za ki-kanda na za kimataifa za haki za binadamu.

Pia mnaweza kuweka katika mkataba vifungu vya namna makubaliano yoyote yanayotokana na utatuzi wa migogoro yatakavyotekelezwa, ikiwemo kuweka tarehe za ukomo wa kurekebisha kasoro au kuanzisha taratibu mpya za ufuatiliaji. Mnaweza pia kuweka kipengele cha kulazimisha kampuni kus-itisha shughuli zake hadi mzozo utatuliwe ikiwa madhara ni makubwa na yanaendelea.

Endapo mchakato wa utatuzi wa migogoro hausuluhishi mzozo uliopo, au mwekezaji harekebishi kasoro mlizoibua, mnaweza kutumia **njia nyingine za kushughulikia malalamiko ambazo ni za kimataifa au za mashirika, zikiwemo**:

- Iwapo mradi utapokea ufadhili wa IFC, mnaweza kufikisha malalamiko yenu kwa Mshauri Msimamizi wa sheria wa IFC.
- Iwapo mradi unafadhiliwa na Benki ya Dunia au benki yoyote ya maendeleo ya kikanda, kila benki pia ina michakato yake ya ndani ya kushughulikia malalamiko.
- Iwapo uwekezaji huo unasimamiwa na mamlaka ya udhibiti yenye taratibu zake za uangalizi, majukwaa ya wadau mbalimbali (kama vile Jukwaa la wazalishaji wa Mafuta ya Mawese au Taasisi ya Uwajibikaji katika Madini), nayo huwa na utaratibu wao wa kushughulikia malalamiko.
- Iwapo mwekezaji anatoka katika nchi mwanachama wa Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), basi OECD imeanzisha vituo maalumu vya Mawasiliano ya Kitaifa vinavyopokea na kufanyia kazi malalamiko.
- Makampuni pia huwa na taratibu zao za ndani za kushughulikia malalamiko: mnaweza kuwasilisha malalamiko yenu kwa bodi ya kampuni.

>> Soma sehemu ya huko juu kuhusu “ikiwa hamjaridhia” kwa ajili ya kuona mikakati mingine mnayoweza kuitumia kuhusiana na ukiukaji unaoendelea wa mkataba.

**Haki ya watu wa asili ya kujiamulia mambo yao wenywe imeainishwa katika mikataba mbalimbali ya kimataifa. Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kuamua kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi ni kipengele muhimu kwa Watu wa Asili katika kulinda na kutetea haki yao ya kujiamulia mambo. Hii ndiyo hoja ya kwanza ya utetezi wakati wawekezaji na maofisa wa serikali wanapokuja na miradi inayoweza kuathiri jamii za Watu wa Asili, ardhi, maeneo na rasilimali zao. Kwa sababu hii, Watu wa Asili wawe tayari kutetea haki yao ya Kujulishwa, Kuelewa na Kuamua kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Watu wa Asili lazima wawe na mwongozo wa kuwasaidia kusimamia haki zao hizo, na wawe tayari kuongoza majadiliano kuhusu haki hizo kwa kutoa masharti yao.**

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO A: MAANA/MANENO MUHIMU

**Faida ya kila mwaka:** Kiasi cha pesa ambacho kampuni ilipata katika kipindi cha mwaka mzima. Taarifa hii inakuwemo ndani ya taarifa ya fedha.

**Haki za pamoja:** Haki za pamoja za Watu wa Asili ni pamoja na kutambua historia yao, lugha, utambulisho na tamaduni zao, na haki ya kutumia na kumiliki ardhi kwa pamoja, maeneo, na maliasili ambayo wamekuwa wakimiliki na kutumia kijadi, pamoja na haki ya kutunza Maarifa yao ya Jadi.

**Haki ya lazima ya kumiliki ardhi:** Ni uwezo wa serikali wa kuwa na haki ya kipekee ya kumiliki ardhi kwa matumizi ya umma, bila ya ridhaa ya wamiliki au wakaaji wake.

**Mkataba:** Inapotokea pande mbili au zaidi zinaahidi kufanya jambo fulani kwa faida fulani, basi uamuzi huo unakuwa sehemu ya mkataba, ambao unawalazimisha kisheria kwa kuweka masharti ambayo yanaweza kutekelezwa kwa amri ya mahakama.

**Mkataba kati ya mwekezaji na jamii:** Mkataba ulioingiwa kati ya jamii na kampuni au mwekezaji unaoweka masharti ya kampuni kuweza kukodisha/kutumia ardhi na rasilimali za jamii.

**Kujiridhisha:** Mchakato au jitihada za kukusanya na kuchambua taarifa kabla ya kufanya uamuzi au kabla ya kuingia makubaliano au mkataba na mhusika mwingine. Ni maamuzi na mipango inayozingatia hatari na hivyo kufanya uamuzi wa ama kuendelea au kutoendelea na mradi na, ikiwa ni hivyo, basi kuamua pia namna ya kupunguza hatari kwa jamii, kiuchumi na kimazingira.

**Haki za kisheria zinazotekelezeka:** Haki zinazotambuliwa na sheria na kulindwa na mifumo na taasisi za kisheria. Haki nyingi zinazotekelezeka zimewekwa katika katiba za nchi na sheria za kitaifa na kimataifa. Pia sheria za watu wa asili au za kimila zinaweza, kwa baadhi ya mazingira, kutekelezwa na Serikali na kutumika mahakamani. Haki za kisheria zinazotekelezeka pia zinaweza kuwekwa kupitia mkataba.

**Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii (ESIA):** Ni ripoti ya uchunguzi wa kitaalamu na uchanganuzi inayobashiri athari za kimazingira na kijamii zinazotokana na mradi na kupendekeza hatua za kupunguza athari hizo zinazoweza kutokea. Kazi hii hufanywa kabla ya utekelezaji wa mradi.

**Ombi la Sheria ya Uhuru wa Habari (FOIA):** Ombi rasmi kwa serikali kupewa taarifa na nyaraka za serikali.

**Utaratibu wa malalamiko:** Mchakato unaotumika na wanajamii kutafuta suluhisho la malalamiko yao kuhusu athari mbaya za mradi au mwenendo wa kampuni (pamoja na wafanyakazi na wawakilishi wa kampuni).

**Haki za binadamu:** Haki zinazopatikana kwa binadamu wote bila ubaguzi, bila ya kujali utaifa, jinsi, jinsia, kabila, rangi, dini, lugha, mahali anapoishi au hadhi nyingine yoyote. Haki za binadamu ni za ulimwengu wote, haziwezi kutenganishwa, hazigawanyiki, zinahusiana, na zinategemeana. Haki za binadamu kwa wote husimamiwa kisheria na mikataba, sheria za kimila za kimataifa, kanuni za jumla na mifumo mingine ya kisheria ya kimataifa.

**Miundombinu:** Majengo na mifumo isiyo ya kujengwa inayohitajika katika nchi, mji, kijiji, au kuendeshea biashara, na miundombinu hiyo ni kama vile mabwawa, madaraja, majengo, barabara, minara ya mawasiliano, mifumo ya umeme, n.k.

**Mradi wa uwekezaji:** Mradi unaotekelezwa kwa ajili ya kutengeneza faida.

**Kukodisha:** Mkataba ambapo upande mmoja unahamisha haki ya matumizi ya ardhi na/au mali zake kwenda upande wa pili kwa muda maalumu kwa malipo ya mara kwa mara.

**Leseni:** Ruhusa, mara nyingi hutolewa na serikali, kwa ajili ya kufanya shughuli maalumu. Leseni zinaweza kuwa za uwindaji, uchimbaji madini, ukataji miti, uvuvi n.k.

**Taasisi za kimataifa:** Taasisi za kimataifa zinaundwa na nchi tatu au zaidi zinazofanya kazi pamoja katika masuala yenye maslahi kwa wote na ya kipaumbele cha kimataifa. Mashirika haya yanaweza kufadhili miradi mbalimbali kwa kutumia fedha za serikali nyingine. Taasisi ya kimataifa huanzishwa kupitia mkataba, azimio, au makubaliano kati ya nchi wanachama zinazoshiriki.

**Majadiliano:** Majadiliano ni mchakato rasmi (unaoweza kuhusisha upande wa tatu usioegemea upande wowote), ambapo watu wawili au zaidi au pande zote hukutana kwa lengo la kufikia makubaliano. Kila upande unawasilisha kile wanachotaka, na masharti ya makubaliano yanajadiliwa hadi mwafaka unapatikana.

**Upande katika mkataba:** Mtu au shirika linaloingia katika mkataba na watu au mashirika mengine.

**Kibali:** Ruhusa, kwa kawaida hutolewa na serikali, wa ajili ya kufanya shughuli maalumu.

**Ugawanaji faida:** Ni utaratibu ambapo mtu wa tatu (kwa mfano, jamii) anapokea moja kwa moja sehemu ya faida ya kampuni.

**Haki ya kupata njia:** Haki ya kisheria, iliyoanzishwa kwa ajili ya kuendelea kutumia au kupita kwenye njia maalumu au mali inayomilikiwa au iliyokodishwa kwa mtu mwingine.

**Kampuni tanzu:** Kampuni tanzu ni ile inayomilikiwa kikamilifu au kwa sehemu na kampuni nyingine. Kampuni mama yanamiliki na kudhibiti hadi asilimi ya hisa za kampuni tanzu, na kuwa udhibiti wa kampuni tanzu.

# KIAMBATISHO B:

# MSINGI WA KISHERIA WA HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI

Haki ya Watu wa Asili ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi iko katika sheria za kimataifa na desturi zake, hasa Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Watu wa Asili, ambalo si la kisheria. Nchi zinazoridhia tamko hilo zinaweza kutunga na kurekebisha sheria zao zinazoakisi vifungu vya tamko hilo katika mifumo yao ya sheria za ndani ya nchi. Benki mbalimbali za kimataifa zimeweka katika sera zao suala la kuzingatia haki ya Watu wa Asili ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi, hata hivyo mara nyingi hawachukui maoni ya Watu wa Asili walioathiriwa. Hatimaye, taasisi na mamlaka mbalimbali ya udhibiti na makundi ya usimamizi huwa na sera na taratibu za ndani zinazotumika kuhakikisha kuwa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi inawekwa kwenye taratibu na viwango. Kiambatisho hiki kinaeleza kwa kifupi sheria na sera hizi. Hata hivyo, kwa sababu kila nchi ina sheria tofauti, tunashauri kwamba utumie kiambatisho hiki kama kianzio cha utafiti wako mwenyewe, kufanya kazi na wanasheria, wasaidizi wa kisheria, mawakili na wanaharakati.

## SHERIA ZA KIMATAIFA NA MIKATABA

**Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi ni utaratibu wa sheria za kimataifa uliowekwa na Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu wa Asili (UNDRIP), Mkataba Na 169 wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), na Mkataba kuhusu masuala ya Bayoanuai CBD).**

Mwaka 2007, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha Azimio la kutambua haki ya kujiamulia mambo yao wenyewe na kutambua rasmi Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kama hitaji la lazima kwa shughuli yoyote inayoathiri ardhi, maeneo na maliasili za Watu wa Asili. Maandishi kamili ya yamechapishwa kwenye kisanduku hapa chini.

Mkataba na 169 wa Shirika la Kazi Duniani (ILO 169), uliopitishwa mwaka wa 1989 (pia unajulikana kama Mkataba wa Watu wa Asili), ulikuwa mkataba wa kwanza wa kimataifa kutambua uhalali wa taasisi za kiuchumi na kisiasa za watu wa asili, pamoja na maendeleo yao ya kiuchumi na kuendeleza utambulisho wao, lugha, dini, maadili na desturi. ILO 169 ina hadhi ya kuwa mkataba na ni hati ya kisheria kwa nchi 23 ambazo zimeuridhia.

## IBARA ZINAZOELEZA BAYANA KUHUSU HAKI YA WATU WA ASILI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI KWENYE TAMKO LA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU HAKI ZA WATU WAASILI

- **Ibara ya 10.** Watu wa Asili hawataondolewa kwa lazima kutoka kwa ardhi au maeneo yao. Hawatahamishwa kwenye makazi yao kabla ya kupewa Haki yao ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kuhusu maisha yao na baada ya makubaliano ya fidia ya haki na, ikiwezekana, wawe na uhuru wa kurejea.
- **Ibara ya 11 (2).** Nchi zitatoa nafuu madhubuti, zikijumuisha utaratibu wa urejeshwaji utakaoandaliwa kwa kuwashirikisha Watu wa Asili, kuheshimu mali zao za kitamaduni, kiakili, kidini na kiroho zilizochukuliwa bila Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi au kwa kukiuka sheria, mila na desturi zao.
- **Ibara ya 19.** Nchi zitashauriana na kushirikiana kwa nia njema na Watu wa Asili kupitia uwakilishi wa taasisi zao ili wapate Haki yao ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kabla ya kupitisha na kutekeleza hatua za kisheria au kiutawala zinazoweza kuwaathiri.
- **Ibara ya 28 (1).** Watu wa Asili wana haki ya kusahihisha, kwa njia ambazo zinaweza kujumuisha urekebishaji au, endapo hili halitawezekana, basi wapewe fidia ya haki, na ya usawa, kwa ardhi, maeneo, na rasilimali ambazo wamemiliki kijadi au wamekalia au kuzitumia, na ambazo zimetwaliwa, kukaliwa, kutumika, au kuharibiwa bila ya wao kupewa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi.
- **Ibara ya 29 (2).** Mataifa yatachukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa hakuna uhifadhi au utupaji wa vifaa vya hatari utakaofanyika katika ardhi au maeneo ya Watu wa Asili bila ya Haki yao ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi.
- Ibara ya 32 (1). Watu wa Asili wana haki ya kuamua na kuandaa vipaumbele na mikakati ya kuendeleza au kutumia ardhi au maeneo yao na rasilimali nyingine. (2) Nchi zitashauriana na kushirikiana kwa nia njema na Watu wa Asili kupitia taasisi zao ili kupata ridhaa yao kabla ya kuidhinishwa kwa mradi wowote unaoathiri ardhi au maeneo yao na rasilimali nyinginezo, hasa kuhusiana na kuendeleza, kutumia au kuchimba madini, kuvuna maji au rasilimali nyingine.

Mkataba wa ILO Na 169 unatambua haki ya Watu wa Asili ya kushauriana nao watakapoathiriwa na miradi ya maendeleo na “na muda wowote inapotokea wameathiriwa moja kwa moja na hatua za kisheria au za kiutawala.” (Ibara ya 6(1)
(a).) Ibara ya 7(1) inasema kwamba “Watu husika watakuwa na haki ya kujiamulia vipaumbele vyao wenyewe kwa ajili ya mchakato wa maendeleo kwa vile unaathiri maisha yao, imani, taasisi na ustawi wao wa kiroho na ardhi wanayomiliki au kutumia, na kusimamia, kadiri inavyowezekana, maendeleo yao ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Aidha, watashiriki katika kuandaa, kutekeleza, na kutathmini mipango na programu za maendeleo ya kitaifa na kikanda ambazo zinaweza kuwaathiri moja kwa moja. Ibara ya 16 inataka watu wa asili wapewe haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi ya kuhamishwa.

**Mkataba kuhusu Masuala ya Bayoanuai** uliosainiwa na serikali 150 mnamo mwaka 1992 wakati wa Mkutano Mkuu uliofanyika Rio na kuridhiwa na nchi 196 mwaka 2015, unalinda maarifa ya jadi ya Watu wa Asili kwa kuruhusu matumizi ya maarifa hayo kwa masharti kwamba lazima watu wa asili waridhie. Mkataba huo unasisitiza waziwazi Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Ibara 8(j) ya CBD inaeleza kuwa, kwa kuzingatia sheria za nchi husika, kila upande unatakiwa:

1. “Kuheshimu, kuhifadhi, na kudumisha maarifa, uvumbuzi, na desturi za jamii za Watu wa Asili zinazoendeleza maisha ya kitamaduni yanayofaa kwa uhifadhi na matumizi endelevu ya bayoanuwai;”
2. “Kuendeleza matumizi yao kwa upana zaidi kwa kuridhia na kuwashirikisha wenye ujuzi, ubunifu na njia nzuri;” na
3. “Kuhimiza usawa katika kugawana faida inayotokana na matumizi ya ujuzi, ubunifu na njia hizo.”

Mpango Kazi wa utekelezaji wa Ibara ya 8(j) ya CBD unaeleza kwamba “upatikanaji wa Maarifa ya Jadi, ubunifu, na njia za utendaji za Watu wa Asili unapaswa kutokana na ridhaa inayotokana na kujulishwa na kuelewa kabla ya wahusika kufanya maamuzi. Sekretarieti ya CBD pia imechapisha miongozo mbalimbali inayolinda haki za Watu wa Asili. Kama sehemu ya mpango kazi wake kuhusu Ibara ya 8(j), pande zote za Mkataba wameandaa miongozo ya hiari kwa ajili ya Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi kuhusiana na michakato ya kupata maarifa ya jadi na kufanya tathmini.

Ushiriki katika hatua zote za maendeleo unatokana na Ibara ya kwanza ya **Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (ICESCR),** ambayo inasema kwamba “Watu wote wana haki ya kujiamulia. Kwa mujibu wa haki hiyo wanaamua kwa uhuru juu ya hali yao ya kisiasa na kufuatilia kwa uhuru maendeleo yao ya kiuchumi, kijamii, na kitamaduni.”

## JE HAKI YA WATU WA ASILI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI INALINDWA NA SHERIA ZA NCHI?

1. **Je nchi yenu imesaini Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wa Asili?**

   KAMA NDIYO: *nchi inabidi iheshimu haki yenu ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla Ya Kufanya Maamuzi.*

   KAMA HAPANA: *mtakuwa na changamoto nyingi katika kupigania haki yenu ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.*

2. **Je kuna sheria yoyote ya nchi inayotambua haki ya Watu wa Asili ya kujulishwa, kuelewa na kukubali kwa hiyari kabla ya kufanya maamuzi?**

   KAMA NDIYO: Ifuatilieni kwa umakini hiyo sheria kujua matakwa yake. Vifungu vya hiyo sheria vinasemaje? Inawahusu akina nani? Sheria inataja taratibu zipi za kufuatwa?

   KAMA HAPANA: Je kuna sheria nyingine ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya kutetea haki ya kujulishwa, kuelewa na kukubali kwa hiyari kabla ya kufanya maamuzi (kama vile sheria za ujenzi au mipango ya matumizi ya ardhi)? Je zinaweza kutumika?

3. **Je kuna mfano wowote wa kesi katika nchi yenu inayotetea Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi?**

   KAMA NDIYO: Mahakama iliamuaje? Je inaweza kutumika pia katika suala lenu?

   KAMA HAPANA: Je kuna kesi yoyote ya mfano katika nchi nyingine ambayo mnaweza kuitumia kama marejeo ya kutetea haki zenu? Je kuna wanajamii wanaochukua hatua za kupinga mradi wa maendeleo katika nchi yenu?

### SHERIA ZA NCHI NA MIKATABA

Iwapo nchi yenu imesaini au kuridhia Azimio, basi inatakiwa kutengeneza sheria za nchi zinaweka vifungu hivyo vya Azimio kuwa sehemu ya sheria za nchi. Miongozo ya nchi kuhusu haki ya kujulishwa, kuelewa na kukubali kwa hiyari kabla ya kufanya maamuzi inaweza kufanyika katika mfumo wa mikataba au makubaliano yanayohusu Watu wa Asili. Jedwali hapo chini lina maswali ya kuwaongoza katika utafiti wenu.

### MIONGOZO YA KIMATAIFA

Mbali na sheria za kitaifa na kimataifa, mashirika kadhaa ya kimataifa na taasisi za fedha, kama vile Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa, na Umoja wa Mataifa, zimeandaa miongozo kwa ajili ya Haki Ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi na wameweka hilo kama takwa muhimu katika sera zao ili kuhakikisha kwamba programu zao na miradi ya maendeleo vnaheshimu haki za watu wa asili. Viwango hivi vinatakiwa kutumika na serikali, makampuni na vyombo vingine vinavyohusika na mipango ya maendeleo ya taasisi. Hata kama nchi yenu haina mwongozo wa HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI, kama mradi wa uwekezaji unafadhiliwa na moja ya mashirika haya, mnaweza kuwataka wawekezaji kuzingatia miongozo ya haki hii (Tazama Sehemu ya 4 kwa maelezo zaidi kuhusu hili).

### MIONGOZO YA SEKTA HUSIKA

Baadhi ya makampuni na makundi au taasisi za kisekta wameanza kujumuisha kanuni za Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi katika sera na taratibu zao za ndani. Mbinu nyingine nyingi za hiari huhitaji makampuni kushauriana na kutafuta ridhaa inapotokea miradi inaathiri haki za Watu wa Asili, kama vile Kiwango Na 7 cha Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), Kanuni za Ikweta, au Mfuko wa Mazingira. Shirikianeni na wanasheria wenu, wasaidizi wa kisheria, na mawakili ili kujua kama mradi uliopangwa ni sehemu ya sekta ambayo ina taratibu za udhibiti, viwango, na taratibu za kuwasilisha malalamiko kwa ajili ya haki yenu ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi. Kwa ujumla, hata hivyo, viwango hivi haviwezi kulinda haki yenu hiyo kuliko Azimio; miongozo ya kisekta inaweza kutumika kusukuma hoja ya mazungumzo na majadiliano yanayozingatia vipaumbele vya Watu wa Asili.

## KIAMBATISHO C: KUKOKOTOA THAMANI YA RASILIMALI ZILIZOMO KWENYE ARDHI NA MIFUMO YA KIIKOLOJIA

Mnaweza kusaidia jamii yenu kwa kufanya zoezi la mara moja la kukokotoa gharama za soko za kufidia thamani ya rasilimali ambazo kwa sasa mnazipata kwa kuwinda, kuokota matunda, au menginevyo kutoka katika ardhi yenu (ambazo hamtaweza kuvipata baada ya kuridhia mradi kwa kutoa ardhi yenu kwa mwekezaji). Zoezi hili linatoa makadirio ya kiasi cha pesa ambacho kila familia ingepata kwa ajili ya kununulia vitu hivyo vya maliasili baada ya kukodisha misitu yenu, ardhi ya malisho au ardhioevu kwa mwekezaji na hamtaweza tena kwenda kwenye maeneo hayo kukusanya chakula, madawa, vifaa vya ujenzi, au rasilimali nyingine muhimu.

Zoezi hili la uthamini linafanywa vyema zaidi kupitia mkutano mkubwa wa hadhara unaohudhuriwa na wanaume, wanawake, wazee, vijana, na watu wanaofanya kazi mbalimbali za kujipatia riziki, wakiwemo wawindaji, wavuvi, na wengine ambao wanafahamu kwa karibu rasilimali zilizomo. Mnaweza kuwaongoza wanajamii kufuata hatua hizi:

- Kwanza, kubangua ubongo na kutaja orodha ya maliasili zote zinazotumika na jamii nzima au zinazopatikana katika misitu ya jumuiya, malisho, ardhi oevu, na njia za maji. Baada ya kuandaa orodha kamili, chagueni rasilimali kati ya 8 -10 zinazotumika zaidi ili muweze kukokotoa thamani yake kwa kila kaya.
- Kadiria ni kiasi gani cha kila rasilimali kinatumiwa au kukusanywa na familia moja ya kwa kila wiki. Tumia “kipimo” ambacho rasilimali hiyo inauzwa kwenye soko la ndani (fungu/ kikapu/ lita/ndoo), kisha uhesabu ni bei ya kila kipimo na kadiria kila familia itatumia kiasi gani cha fedha kununulia vitu hivyo kwa wiki au mwezi.
- Kadiria bei ya kipimo kimoja cha maliasili hizo katika soko lenu.
- Piga hesabu ni kiasi gani kila familia italazimika kutumia kuvinunua vitu hivyo kila wiki, mwezi, na mwaka. Ikiwa rasilimali inatumiwa mara moja kwa mwezi au mara moja kwa mwaka, ruka hesabu ya kila wiki na ujaze gharama tu kwa mwezi au mwaka.
- Kadiria idadi ya familia katika jamii yenu, kisha zidisha kwa gharama ya kila kitu ili upate wastani wa gharama kwa familia ingetumia.
- Hatimaye, hesabu jumla ya kiasi ambacho jumuiya ingelazimika kutumia kununua mahitaji haya ya msingi ya kaya sokoni, kwa kutumia sarafu ya taifa na dola za Marekani (sarafu inayotumiwa na wawekezaji).

Chati ifuatayo inaonesha namna kufanya zoezi hili. Safu ya kwanza imejazwa kama mfano. Chati inaweza kuchorwa kwenye kipande kikubwa cha karatasi ili wanajamii waweze kuona na kufuatilia ukokotoaji wa hesabu. Mara baada ya kukokotoa thamani ya kile ambacho jamii yenu inakusanya kutoka kwenye ardhi yenu kila mwaka, mnaweza kuingia kwenye mazungumzo kuhusu HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI na kufahamu zaidi kuhusu thamani ya fedha ya mali zenu na namna ya kutoza kodi, endapo mtakuwa mmeridhia.

| **(Washiriki wanaamua ni rasilimali zipi za kuorodheshwa katika safu wima ya kushoto, lakini wawezeshaji wanapaswa kupendekeza mifano hii au mingine kama washiriki hawajapendekeza.)** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Zinazokusanywa na familia moja kwenye ardhi na maji ya pamoja** | **Kipimo** (fungu, kilo, nk.) | **Kipimo kinachotosha kwa wiki** | **Bei ya kipimo kimoja** | **Ghara ma ya wiki** | **Ghara ma ya mwezi** (x4) | **Ghara ma ya mwaka** (x12) |
| **Kuni** | **Fungu moja** | **7** | **$1** | **$7** | **$28** | **$336** |
| **Maji** | | | | | | |
| **Nyama ya porini** | | | | | | |
| **Samaki** | | | | | | |
| **Mboga #1** | | | | | | |
| **Mboga #2*** | | | | | | |
| **Dawa ya mitishamba** | | | | | | |
| **Matunda ya porini #1*** | | | | | | |
| **Matunda ya porini #2** | | | | | | |
| **Nyasi za kuezekea nyumba** | | | | | | |
| **Gharama za jumla na rasilimali zinazotumika na familia moja** | | | | | | ○ |

* Ongeza mstari mwingine kama kuna aina zaidi za mboga, matunda ya porini, asali, vifaa vya ujenzi nk.

– lakini hakiki mnakokotoa vitu vile vinavyotumika kwenye kaya pekee.

| Ghrama ya jumla ya vyakula na rasili-mali nyingine kwa familia moja | Idadi ya familia katika jamii yenu | Ghrama ya jumla kwa jamii nzima kwa |
|---|---|---|
| | X | = |

# KIAMBATANISHO D: MAONO YA MUSTAKABALI WA JAMII YENU

Jamii yenu inaweza kuwa na utamaduni wake wa kuwa na maono na kupanga mambo yajayo. Kwa jamii ambazo hazina huu utamaduni ni vema zikawa nao. Ni vyema kuwa na zoezi hili kwa pamoja, kwa kutoa nafasi kwa wanaume, wanawake, wazee, na vijana kutoa mawazo yao. Mchakato huu unaweza kuchukua kama saa mbili hadi tatu, au kwa wiki kadhaa.

**Hatua ya 1: Kukumbuka zamani.** Waombe wanajamii waeleze jinsi ardhi yao, maliasili, na mahusiano ya kijamii yalivyokuwa miaka 40-50 iliyopita, wakati huo wazee wa leo walikuwa watoto. Waombe wazee waeleze wanachokumbuka cha wakati huo. Andika wanachosema. Baadhi ya maswali ya kuhamasisha majadiliano yanaweza kujumuisha:

- Mandhari ya wakati huo ilikuwaje? Je, ubora wa ardhi, maji na hewa ulikuwaje?
- Je, watu walikuwa wanapata nini kwenye ardhi yenu? Maliasili hizi zilikuwa nyingi kiasi gani?Ilichukua muda gani kukusanya rasilimali hizi?
- Je, watu waliishi na kufanyaje kazi pamoja ndani ya jamii?
- Ni shughuli za kitamaduni, matambiko, au sherehe zilifanyikaje?
- Miundo ya kiutawala ilikuwaje na ilifanyaje kazi?

*Jamii yenu inaweza pia kutengeneza ramani ya hali ya mazingira ya wakati wa zamani: Misitu ilikuwa na ukumbwa gani? Ni mimea gani ilikua? Ni wanyama gani walikuwa wengi? Ni mimea gani iliyopatikana kwa urahisi? Ni maeneo gani yalikuwa na maji mengi?*

**Hatua ya 2: Kutafakari hali ya sasa.** Waombe wanajamii kutafakari hali ya ardhi yao, maliasili, na mahusiano ya jamii yalivyo kwa sasa. Baadhi ya maswali ya kuhamasisha majadiliano yanaweza kuwa:

- Je, kwa sasa rasilimali ambazo watu hukusanya zinapatikana kwa kiasi gani?
- Watu wanaishije na kufanyaje kazi pamoja ndani ya jamii?
- Shughuli za kitamaduni, matambiko na sherehe zinafanyikaje?
- Je, kwa sasa jamii yenu inafanyaje maamuzi kuhusu ardhi na maliasili? Je maamuzi na kanuni zinasimamiwaje kwa sasa? Je, viongozi wanasimamia ardhi yenu vizuri?

*Jamii yenu inaweza pia kutengeneza ramani ya hali ya mazingira ya wakati wa zamani: Misitu ilikuwa na ukumbwa gani? Ni mimea gani ilikua? Ni wanyama gani walikuwa wengi? Ni mimea gani iliyopatikana kwa urahisi? Ni maeneo gani yalikuwa na maji mengi?*

**Hatua ya 3: Itakavyokuwa siku za mbeleni.** Kisha, waulize wanajamii wanavyofikiri jinsi ardhi yao na maliasili/mahusiano ya kijamii yatakuwaje miaka 40-50 kutoka sasa, kwa wajukuu zao, kama mambo yataendelea kuwa kama yalivyo leo. Waombe washiriki wafumbe macho wajaribu "kuona" maono katika mawazo yao. Wape muda wa kufikiri juu ya hili. Usiharakishe hatua hii - inaweza kuibua hisia katika mioyo yao. Waombe waeleze walichokiona kwenye maono yao kuhusu itakavyokuwa. Andika wanachosema. Baadhi ya maswali ya kuhamasisha majadiliano yanaweza kuwa:

- Mandhari itakuwaje? Je, hali ya maji, udongo na hewa ikoje?
- Je, upatikanaji wa maliasili utakuwaje?
- Je, watu wataishije na kufanya kazi pamoja? Watu watajipatiaje riziki zao?
- Nani ataendeleza mila zenu?

**Hatua ya 4: Hali ya baadaye mnayotamani.** Waombe wanajamii kufumba macho yao mara ya pili na kuwaza kuhusu ulimwengu wanaotamani wajukuu wao waukute miaka 40 au 50 kuanzia sasa. Tena, ruhusu dakika chache kufikiria hili kwa ukimya, kisha waombe weleze maono yao. Andika kwenye kipande kikubwa cha karatasi kila kitu wanachoeleza. Uliza maswali yale yale ya hapo juu, na mengine yoyote unayofikiria yanafaa.

***Jamii yenu inaweza pia kutengeneza ramani ya hali ya mazingira ya baadaye.*** *Mambo gani mngependa kama jamii kuyafanya kwa ajili ya kutengeneza maisha bora ya baadaye hasa katika masuala ya bayoanuwai, upatikanaji wa maji, ukubwa wa misitu nk?*

**Hatua ya 5. Unganisha zoezi la hali ya baadaye mnayotamani na Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi.** Ukishaelewa yaliyopita ya jamii yenu na taswira kamili ya jinsi mngependa jamii yenu iwe siku zijazo, mnaweza kuongelea Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari Kabla ya Kufanya Maamuzi kwa kuweka wazi malengo, maslahi na mahitaji ya jamii yenu. Hii inaweza kuwasaidia wakati wa majadiliano na mazungumzo kati yenu na wawekezaji na maofisa wa serikali.

## KIAMBATISHO E:
ORODHA YA MASHIRIKA NA TAASISI ZA KIMATAIFA AMBAZO WATU WA ASILI WANAWEZA KUWASILIANA KWA MSAADA ZAIDI

**Mashirika yafuatayo yalichangia katika kuandaa mwongozo huu.** Tafadhali jisikieni huru kuwauliza maswali yoyote moja kwa moja kwao. Kwa usaidizi wa kisheria au kiufundi, tunashauri mtafute msaada kutoka kwa mashirika ya ndani, ya kikanda, na/au ya kimataifa yenye uzoefu wa kufanya kazi na Watu wa Asili na katika majadiliano kuhusu HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI. Ingawa mashirika yetu hayawezi kutoa ushauri wa kisheria, yanaweza kuwaunganisha na mashirika yanayoweza kuwasaidia kisheria.

**Cultural Survival**
www.culturalsurvival.org
Contact: culturalsurvival@cs.org

**First Peoples Worldwide**
www.colorado.edu/program/fpw
Contact: fpw@colorado.edu

**Batani Foundation**
www.batani.org
Contact: info@batani.org

**Securing Indigenous Peoples Rights in the Green Economy (SIRGE) Coalition**
www.sirgecoalition.org
Contact: https://www.sirgecoalition.org/contact-us

### MIFUMO YA KIMATAIFA NA MASHIRIKA YA KIMKATABA

**United Nations Permanent Forum on Indigenous Issues (UNPFII):** social.desa.un.org/issues/indigenous- peoples/unpfii

**Expert Mechanism on the Rights of Indigenous Peoples (EMRIP):** www.ohchr.org/en/hrc-subsidiaries/expert- mechanism-on-indigenous-peoples

**United Nations Special Rapporteur on the Rights of Indigenous Peoples:** www.ohchr.org/en/ special-procedures/sr-indigenous-peoples

**Inter-American Commission on Human Rights (IACHR),** Rapporteurship on the Rights of Indigenous Peoples https://www.oas.org/en/iachr/jsForm/?File=/en/iachr/r/DPI/default.asp

**Organization of American States (OAS)**
https://www.oas.org/en/

**International Labour Organization (ILO)** https://www.ilo.org/global/topics/indigenous-tribal/lang-- en/index.htm

**Committee on the Elimination of All Forms of Racial Discrimination (CERD)**
https://www.ohchr.org/en/treaty-bodies/cerd

**Committee on the Elimination of Discrimination Against Women (CEDAW)**
https://www.ohchr.org/en/treaty-bodies/cedaw

### MASHIRIKA YA KIMATAIFA YENYE VIWANGO VINAYORUHUSU HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI; VIUNGO KWA AJILI YA KUWASILISHA MALALAMIKO

Kama ilivyoelezwa katika mwongozo, ikiwa haki zenu za kufanya maamuzi zimekiukwa, **kuna mifumo mbalimbali ya kimataifa na ya mashirika ambayo jamii yenu inaweza kufikisha malalamiko yenu, na hilo litategemea nani anayefadhili mradi au wapi shirika la mwekezaji limesajiliwa,** ikiwa ni pamoja na:

**The International Finance Corporation Compliance Advisor Ombudsman:** https://www.cao-ombudsman.org/

**The World Bank's Grievance Redress Mechanism:** https://www.worldbank.org/en/projects-operations/products-and-services/grievance-redress-service

**The African Development Bank:** https://www.afdb.org/en/independent-rmechanism/management-of-complaints/how-to-file-a-complaint

**The Asian Development Bank's Accountability Mechanism:** https://www.adb.org/who-we-are/ accountability- mechanism/how-file-complaint

**The Inter-American Development Bank's Grievances Portal** *(In English, Spanish, and Portuguese):* https://www.iadb.org/en/projects/grie

**The European Bank for Reconstruction and Development:** https://www.ebrd.com/ipam

**The Roundtable on Sustainable Palm Oil Grievance Mechanism:** https://askrspo.force.com/Complaint/s/

**The Organization for Economic Cooperation and Development National Contact Points that hear and resolve grievances:** https://www.oecdwatch.org/how-tofile-a-complaint/

# KIAMBATISHO F:
# ORODHA YA MAREJEO

### SHERIA MUHIMU ZA KIMATAIFA:

**Chapisho zima la Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Watu wa Asili:**
https://www.un.org/development/desa/IndigenousPeoples/wp-content/uploads/sites/19/2018/11/UNDRIP_E_web.pdf

**Chapisho zima la Mkataba 169 wa Shirika la Kazi Duniani:**
https://www.ilo.org/dyn/normlex/en/f?p=NORMLEXPUB:55:0 ::NO::P55_TYPE,P55_LANG,P55_DOCUMENT,P55_NODE: RE_en,C169,/Document

**Chapisho kamili la Mkataba kuhusu Bayoanuwai (*Tazama hasa Ibara ya 8j*):**
https://www.cbd.int/convention/text/

### MIONGOZO KUHUSU HAKI YA KUJULISHWA, KUELEWA NA KUKUBALI KWA HIYARI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI NA RIPOTI ZAKE:

**Mkataba wa Bayonuai MO'OTZ KUXTAL voluntary guidelines on FPIC:** https://www.cbd.int/doc/publications/8j-cbd-mootz-kuxtal-en.pdf

**Muongozo wa Kitaalam wa Shirika la Chakula Duniani:** https://www.fao.org/fileadmin/user_upload/partnerships/do cs/ 00000_FPIC_Toolkit_Technical_Guide_FPIC-VGGT-IPs_EN.pdf

**Muongozo wa shirika la Oxfam:** https:// www.culturalsurvival.org/sites/default/files/guidetofr eepriorinformedconsent_0.pdf

**Report summarizing analysis of dozens of Indigenous Peoples' FPIC protocols:** https://enip.eu/FPIC.pdf

**Mwongozo wa uwajibikaji kwa ajili ya wajibu wa kampuni kutekeleza wajibu wa kutoa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi kwa Watu wa Asili na Jamii za Asili:** https://accountability-framework.org/fileadmin/uploads/afi/ Documents/Operational_Guidance/OG_FPIC-2020-5.pdf

### MIONGOZO YA KUJADILIANA MIKATABA NA WAWEKEZAJI NA SERIKALI

**Miongozo miwili kwa ajili ya kuzisaidia jamii za asili kujadiliana masuala ya mikataba na wawekezaji:** https:// namati.org/resources/community-investor-negotiation- guide-1preparing-in-advance-for-potential-investors/ https://namati.org/resources/community-investor- negotiation-guide-2negotiating-contracts-with-investors/

**Primer ya Mkataba wa uwekezaji na namna inavyopuuza haki za kijamii:** https://ccsi.columbia.edu/content/primer- international-investment-treaties-and-investor-state-dispute- settlement

### MIONGOZO YA TATHMINI ZA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII

**Akwé Kon: Voluntary guidelines for the conduct of cultural, environmental, and social impact assessments within Indigenous Communities:** https://www.cbd.int/doc/ publications/akwe-brochure-en.pdf (available in many languages)

### MAREJEO KATIKA LUGHA YA KIRENO

**MPF - Protocolo de Consulta Prévia (State - Justice Department)**
https://www.mpf.mp.br/atuacao-tematica/ccr6/documentos-epublicacoes/protocolos-de-consulta

**OBSERVATÓRIO DE PROTOCOLOS AUTÔNOMOS (Academic and NGO)**
https://observatorio.direitosocioambiental.org/

**Protocolo de Consulta aos Povos e Comunidades Tradicionais (PCTs): o que é e qual sua importância? (NGO)** https://guaicuy.org.br/protocolo-de-consulta-pcts-importancia/#:~:text=Trata%2Dse%20de%20um%20documento,sua%20hist%C3%B3ria%2C%20cultura%20e%20costumes.

**PROTOCOLOS AUTÔNOMOS DE CONSULTA E CONSENTIMENTO: UM OLHAR SOBRE O BRASIL, BELIZE,** CANADÁ E COLÔMBIA **https:// institutoiepe.org.br/wp-content/uploads/2022/03/2022-Livrossobre-Protocolos-de-Consulta-RCA.pdf**

**Protocolos de consulta de diferentes povos indígenas na Amazônia são instrumentos de luta pelos direitos. Entrevista com Angela Amankawa Kaxuyana (Interview)** https://www.ihu.unisinos.br/categorias/186 noticias- 2017/570148-hidreletrica-inunda-cachoeira-sagradaretira- urnas-indigenas-e-gera-crise-espiritual-na-amazonia

### Protocolos de Consulta (Examples):

**Munduruku People -** https://cimi.org.br/wp- content/uploads/ 2021/12/protocolo-consulta-aldeia-takuara- munduruku.pdf

**Quilombola People of Santa Rita -** https:// observatorio.direitosocioambiental.org/wp- content/ uploads/2022/06/Protocolo-de-consulta- quilombola_-SANTA-RITA.pdf

## MAREJEO KWA LUGHA YA KIHISPANIA

**PROTOCOLOS AUTONÓMICOS DE CONSULTA PREVIA INDÍGENA EN AMÉRICA LATINA**
https://www.iwgia.org/images/documentos/Protocolos_Aut onmicos_de_Consulta_Previa_Indgena_en_Amrica_Latina.pdf

**Perspectiva empresarial sobre la consulta previa del C169 en América Latina Lecciones aprendidas** https:// www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---ed_dialogue/--- act_emp/ documents/publication/wcms_820525.pdf

**INCUMPLIMIENTO DE LOS PROTOCOLOS AUTÓNOMOS DE CONSULTA DURANTE EL COVID-19**
https://www.debatesindigenas.org/notas/73-incumplimiento- protocolo-consulta-brasil.html

**Implementación de la consulta y consentimiento previo, libre e informado Experiencias comparadas en América Latina y discusiones sobre una ley de consulta en México** https://www.dplf.org/sites/default/files/ informe_sobre_cons ulta_y_cpli_mexico_final_web.pdf

**El derecho a la consulta previa en América Latina Del reconocimiento formal a la exigibilidad de los derechos de los pueblos indígenas** https:// redjusticiaambientalcolombia.files.wordpress.com/20 11/08/ el_otro_derecho_40_-consulta-previa.pdf





Jamii ikijifunza kuhusu mnyororo wa uwekezaji kwa ajili ya kujifunza maeneo nyeti ya kuweka shinikizo kwa ajili ya uchechemuzi.

# KUPIGANIA HAKI YA WATU WA ASILI YA KUJIAMULIA MAMBO YAO

Mwongozo wa Haki ya Kujulishwa, Kuelewa na Kukubali kwa Hiyari kabla ya Kufanya Maamuzi



Cultural Survival

First Peoples Worldwide University of Colorado Boulder

SIRGE Coalition

Batani

Earthworks

Gesellschaft für bedrohte Völker